**MWILI** wa RAS wa Kilimanjaro waagwa, Ummy aainisha upekee

UKURASA 3

**RAIS** wa Guinea Bissau kuzuru nchini siku tatu, kutembelea SGR

UKURASA 5



**KIPINDUPINDU** chaua wawili Lupaso, Masasi

UKURASA 8



**JUVENTUS, LAZIO ZAMUWANIA GREENWOOD**

UKURASA 22


# Nipashe

Ijumaa Juni 21, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581714

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## MAUAJI WENYE UALBINO

# Waziri Mkuu atangaza vita

**RASMI** opereshеni maalum kila halmashauri...

*Endelea ukurasa 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na viongozi wa Chama cha Watu Wenye Ualbino, ofisini kwake, Mlimwa, jijini Dodoma, jana. Wa (pili kulia) ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Deogratius Ndejembi na (wa tatu kulia) ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga. **PICHA: OWM**


## Mbowe, Lissu kunguruma jukwaa moja kwa wiki tatu wakitumia helikopta

UKURASA 2



Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu



## Joto laua mahujaji 900, kati yao, 800 kutoka Misri

UKURASA 19

**MICHEZO** BODI YA LIGI KUU KUJA NA DAWA WAMILIKI TIMU ZAIDI YA MBILI UK 24

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Amon Kakwale, akiwaongoza askari kufanya usafi katika Soko kuu la Singida mjini jana, kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma, iliyoanza Juni 16 ambayo kilele chake ni kesho kutwa Juni 23. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Waziri Mkuu atangaza vita

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ametoa maagizo kusaidia kuongeza usalama kwa watu wenye ualbino nchini na kukomesha vitendo vya unyanyasaji na mauaji dhidi yao.

Alitoa maagizo hayo bungeni jana wakati wa kipindi cha maswali ya papo hapo kwa Waziri Mkuu.

Ni baada ya Mei 31, mwaka huu kutokea tukio la kutekwa kwa mtoto Asiimwe Novati (mwenye ualbino) aliyekuwa na umri wa miaka miwili na nusu mkazi wa kitongoji cha Mbale, kijiji cha Mulamula, Kata na Tarafa ya Kamachumu, Wilaya ya Muleba, Mkoa wa Kagera nyumbani kwao Kebyera.

"Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe mosi Juni, 2024 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, walithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

"Mtoto huyo alikuwa na mama yake wakati walipovamiwa na vijana wawili majira ya saa 2:15 usiku ambapo mmoja alimkaba koo mama yake ambaye alikuwa nje ya nyumba na mwingine aliingia kwa haraka ndani na kumchukua mtoto na kutokomea naye kusikojulikana," alisema.

Waziri Mkuu alisema, ili kuzuia unyanyasaji na mauaji ya watu wenye ualbino, mamlaka za mikoa na serikali za mitaa zinawajibika katika usimamizi, ulinzi na utoaji wa huduma kwa watu wenye ualbino.

"Hivyo basi, wakuu wa mikoa na wilaya hakikisheni kila halmashauri inaanzisha operesheni maalum za ulinzi kwa watu wenye ualbino," alisisitiza.

Aidha, alisema operesheni hizo zihusishe vikosi vya usalama ili kuhakikisha ulinzi wa watu wenye ualbino dhidi ya mashambulizi na vitisho.

Vile vile, alisema mamlaka za mikoa na wilaya zihamasishe ushiriki wa jamii katika ulinzi na haki za watu wenye ualbino.

Alikumbusha wajibu wa wazazi kwa watoto wao ni kuwapa malezi bora yatakayowawezesha kuwa watu wema katika jamii ambayo wataweza kuitawala dunia.

Amesema viongozi wa dini wana jukumu kwenye suala la kukemea maovu yanayotendeka kwenye jamii hususan mauaji ya watu wenye ualbino nchini kunaonesha upotofu wa maadili na kukosa hofu ya Mungu.

"Vitendo hivyo vinapaswa kukemewa kwa nguvu na nitumie nafasi hii kuwaomba viongozi wetu wa dini tuungane pamoja katika kupambana na mauaji haya ya watu wasiokuwa na hatia hata kidogo.

"Hivyo, niwasihi watumie majukwaa yao ya ibada kuwahubiria waumini wao kuachana na vitendo hivyo vya ukatili ambavyo hata Mwenyezi Mungu anavikataza, watu wenye ualbino wana haki ya kuishi kama walivyo watu wengine," alisema. Akiwageukia waganga wa jadi, alisema wanayo nafasi kubwa ya kutoa mchango wao katika mapambano na vita hiyo ya kuwalinda wenye ualbino.

"Ni wajibu wao kushiriki kukemea vitendo hivi vya mauaji na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuheshimu na kuthamini maisha ya kila mtu, bila kujali hali ya maumbile yake," alisema. Aliagiza waganga wa jadi nchini kushiriki kikamilifu katika kampeni za kupinga mauaji ya watu wenye ualbino. "Wakati umefika kwenu nyote kushirikiana na serikali katika kutokomeza imani potofu zinazochangia mauaji haya. Ninawasihi sana elezeni wazi kwamba hakuna tiba wala mafanikio yanayoweza kupatikana kwa kutumia viungo vya watu wenye ualbino, badala yake matendo haya yanavunja haki za binadamu na kumomonyoa utu wetu kama Taifa," alisema.

Alisisitiza kuwa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala lifanye usajili wa waganga wa jadi na vituo vyao sambamba na aina ya huduma wanayoitoa kwa wateja wao ili kudhibiti huduma holela isiyofuata misingi ya utu na haki za binadamu.

Majaliwa alitoa wito kwa kwa Chama cha Waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala Tanzania (CHAWATIATA) kiwakatae na kuwatenga waganga wanaotumia njia za imani potofu, ramli chonganishi ikiwamo kutoa masharti ya kufanya mauaji ya watu wenye ualbino ili kufanikisha mahitaji ya wateja wao. "Vile vile, toeni taarifa kwa mamlaka husika ili hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao."

Alisema kutokana na nafasi yao ya pekee, waliyonayo viongozi wa kimila amewasihi kutoka kila kona ya Tanzania, washiriki kikamilifu kukemea na kupinga mauaji ya watu wenye ualbino. "Ninawaomba viongozi wetu wa kimila wakiwamo machifu washirikiane na serikali kwa kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama pindi wanapopata fununu za mipango au vitendo vya mauaji ya watu wenye ualbino katika maeneo wanayoishi," alisema.

Jeshi la Polisi pia limetakiwa kuchukua hatua za haraka linapopata fununu ya uwapo wa njama za utekaji na mauaji ya watu wenye ualbino.

"Kuendelea kufanya operesheni ya kuwakamata wote waliotajwa na watakaotajwa kuhusika kwenye matukio ya aina hii kwa lengo la kuua mtandao mzima wa wahalifu hawa na operesheni hizo ziwe endelevu, polisi jamii ishirikishwe kikamilifu ili kupata taarifa zote muhimu katika maeneo husika na watoa taarifa wote walindwe ipasavyo," alisema Majaliwa.


Victoria Finance

Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwanga Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O.Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | NYARAKA YA UMILIKI NA SEHEMU | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PHILIPO RAPHAEL KOMBA | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI MALI YA PHILIPO RAPHAEL KOMBA YENYE NAMBA;SQT/MZ 'B'/123 INAPATIKANA MANZESE 'B'- WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO | J&J RECOVERIES | 26-06-2024 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

MASHARTI YA MNADA;
- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa kama ilivyo.


# Mbowe, Lissu kunguruma jukwaa moja wiki tatu wakitumia helikopta

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA); Freeman Mbowe na Makamu wake, Tundu Lissu, kuanzia kesho wataanza mikutano mfululizo wiki tatu katika mikoa ya Kaskazini wakitumia helikopta.

Ni ziara waliyoibatiza kijeshi 'Operesheni GF' itakayoongozwa na mwenyeji wao, Godbless Lema, Mwenyekiti wa Kanda ya Kaskazini, taarifa iliyotolewa jana na CHADEMA inaeleza.

Ziara hiyo inatarajiwa kugusa majimbo zaidi ya 30, ikipewa jina la 'Operesheni GF'. Mikoa ya Kanda ya Kaskazini ni Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Manyara.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Amani Golugwa, alisema jana kuwa operesheni hiyo inalenga kujenga chama katika mikoa hiyo.

Alisema kuwa katika majimbo ya Ngorongoro na Karatu kutafanyika mikutano mitano, kila jimbo na viongozi wote wakuu, Mbowe na Lissu wanatarajia kunguruma kwenye jukwaa moja.

"Kwa majimbo ya Ngorongoro na Karatu tunatarajia kufanya mikutano mitano katika majimbo hayo, na kwa upekee Mwenyekiti wa Taifa (Mbowe) atashirikiana na Makamu Mwenyekiti Lissu," alisema Golugwa.

Katibu huyo alisema operesheni hiyo inatarajiwa kuanzia Jimbo la Karatu, mkoani Arusha, na kwamba katika majimbo mengine, mikutano hiyo itaongozwa na Mbowe na Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema.

Golugwa alisema kwa sasa wanaendelea kukamilisha maandalizi ya operesheni hiyo.

"Kaulimbiu yetu tunataka kuonesha Watanzania kwa ujumla kwamba tuna watu, tuna Mungu, tuna nguvu. Hiyo ndiyo fahari yetu na uimara wetu Kanda ya Kaskazini ambayo ni ngome ya CHADEMA.

"Tunaendelea na maandalizi ikiwamo kupeleka barua ya vibali vya mkutano, ndege kuruka na masuala mengine," Golugwa alisema.

Katibu huyo alisema operesheni hiyo inafanyika baada ya kumaliza vikao vya mashauriano ndani ya chama vilivyofanyika katika mikoa hiyo ya Kanda ya Kaskazini.

Hii ni operesheni ya kwanza ambayo ni maalum kwa ajili ya kujenga chama hicho, ukiacha maandamano ambayo kilifanya mfululizo yaliyolenga kudai haki katika mambo kadhaa ikiwamo upatikanaji Katiba Mpya, Tume Huru ya Uchaguzi na mabadiliko ya sheria mpya za uchaguzi.

Maandamano hayo yalifanywa na chama hicho katika majiji na miji mikubwa nchini, awamu hii polisi wakiimarisha ulinzi kwa waandamanaji. Si kuwapiga mabomu ya machozi ilivyokuwa imezoeleka zamani.

HABARI KITAIFA

# Mwili wa RAS Kilimanjaro waagwa, Waziri Ummy aeleza upekee wake

**Na Mary Mosha**

WAZIRI wa afya, Ummy Mwalimu, amesema wema na uadilifu wa aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Tixon Nzunda kwa Watanzania na taifa lake, unamfanya ashindwe kumwelezea alikuwa mtu wa aina gani.

Akizungumza jana katika Mji wa Moshi, wakati wa ibada ya kuuaga mwili wa Dk.Nzunda, Waziri Ummy alisema kiongozi huyo ameacha pengo kubwa kwa nchi.

Dk. Nzunda (56) na dereva wake, Alphonce Edson (54), walipoteza maisha kwa ajali ya gari Juni 18 mwaka huu saa 8:30 mchana katika eneo la Mjohoroni (Palestina), Kata ya KIA, Wilaya ya Hai, baada ya gari lake aina ya Toyota Landcruiser GXR, lenye namba STM 7476, kugongana uso kwa uso na lori aina ya Scania lenye namba za usajili T 655 ABY, mali ya Kampuni ya Orange Gas.

Walikuwa wanakwenda Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) kumpokea Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango aliyekuwa anakwenda mkoani Arusha.

Waziri Ummy alisema, "Nimeshindwa kuelezea wema wake kwangu na kwa taifa la Tanzania katika nyadhifa mbalimbali alizoshika hasa kwa kuhudumia wananchi wa Tanzania."

Mwili wa Dk. Nzunda ulisafirishwa jana jioni kutoka Kilimanjaro kwenda nyumbani kwake Goba, wilayani Ubungo, Dar es Salaam kabla ya kwenda kuzikwa kijijini kwao Mpemba-Momba, wilayani Mbozi, mkoani Songwe Juni 22. Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema kifo cha Dk. Nzunda ni pengo lisilozibika kwa sasa na ni ngumu kusema chochote na hajui ataanzia wapi kutokana na utendaji, ushauri na uwajibikaji wake katika mkoa huo.

"Sijui mafaili nitayapeleka wapi, maana wakati wote tulikuwa tuna ushirikiano mkubwa sana. Tunasaidiana kama ndugu na siyo viongozi, Nilikuwa nikimwomba ushauri, alikuwa akinitia moyo na hakukuwa na gumu lililoshindikana kwake, hakika sijui nitaanzia wapi.

"Sijaanza kufanya naye kazi Mkoa wa Kilimanjaro, bali maeneo mbalimbali hasa nikiwa Manyara. Sisi tulikuwa zaidi ya ndugu, tunafanya kazi kwa umoja na ushirikiano.

"Taarifa za kifo chake nilizipokea kwa masikitiko makubwa sana, sikukuu ya Eid el-Adha tulikuwa pamoja, yeye na watoto wake.

"Ninashindwa kuelezea nini niseme. Tulikuta mkoa umeyumba, ila tulishaanza kuunyosha ikiwa ni pamoja na kumaliza urasimu wote," alisema Babu.

Aliitaka familia kuhakikisha inaishi yale aliyoyaishi Dk. Nzunda na kuleta mabadiliko kwenye jamii kama ilivyokuwa adhima yake.

Akizungumza kwa niaba ya wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mbunge wa Hai (CCM), Saashisha Mafue, alisema Dk. Nzunda atakumbukwa kwa kuwa mtu wa haki na kusogeza maendeleo ya mkoa, kutokomeza urasimu na kutafuta majibu ya kila tatizo.

"Familia, Mungu awatie nguvu maana mlikuwa na baba wa mfano, alitokomeza urasimu, alisukuma maendeleo, alikuwa mwadilifu na makini kwenye kazi, hivyo tunaomba tuige na kuleta mabadiliko," alisema Saashisha.

Akitoa salamu, Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Missaile Musa, alisema: "Tulipokea kwa masikitiko sana msiba huu, alikuwa ni mtu wa ushirikiano, upendo na mwelekezaji wa kila mara. Tuliweka mipango mingi. Hakika tumepoteza kiungo muhimu kwa makatibu tawala nchi nzima.

"Tumefanya naye kazi nyingi tu, alikuwa mshauri mwema, hakuwahi kunyanyua mabega licha kuwa na vipaji vingi. Alikuwa na misimamo isiyoyumbishwa. Alikuwa anapenda watu, siyo mchoyo."

## Polisi wawaachia kwa dhamana waandishi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limewaachia kwa dhamana waandishi wa habari watatu lililoshikilia tangu Juni 13 mwaka huu.

Waandishi hao ni mmiliki wa Dima Tv, Dina Maningo na wenzake wawili, Mwanga Wachu na Costantine Mathias, waliokamatwa usiku mkoani Mara na kusafirishwa kwenda jijini Mwanza.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza, Edwin Soko, alisema jana jijini hapa kuwa Maningo na wenzake waliachiwa kwa dhamana jana saa 10 jioni baada ya kukamilisha masharti ya dhamana.

"Dina alishikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kutumia nyaraka za siri za jeshi hilo za tuhuma zinazomkabili aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda, anayedaiwa, kumwingilia kinyume cha maumbile binti mwenye umri wa miaka 21, mwanafunzi wa moja ya vyuo vikuu vya Kanda ya Ziwa.

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) inaelekeza kuwa askari polisi baada ya kuwa wamekamata mtuhumiwa, wanapaswa kumfikisha mahakamani ndani ya saa 24 tangu walimpomkamata au kumwachia huru, isipokuwa kwa makosa yanayohusiana na adhabu ya kifo.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# BRELA yataka wenye viwanda vidogo kujisajili watambulike

**Na Restuta James,**
MOROGORO

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umewataka wenye viwanda vidogo na vya kati kujisajili ili watambulike kitaifa na kimataifa na kufikia masoko makubwa, huku gharama ya kutimiza takwa hilo la kisheria ikianzia Sh. 10,000 inayolipwa mara moja katika uhai wote wa kiwanda.

Akizungumza wakati wa mafunzo ya waandishi wa habari mjini hapa jana yaliyoandaliwa na BRELA, Mkurugenzi wa Leseni wa wakala huo, Andrew Mkapa, alisema watu wengi wanakosa fursa za kuyafikia masoko makubwa yanayotokana na makubaliano ya kimataifa yanayoingiwa na nchi kwenye jumuiya za kikanda na kimataifa kutokana na kutokujisajili.

Alisema Sheria ya Taifa ya Usajili na Leseni za Viwanda, Sura ya 46, imeweka viwanda katika makundi mawili ya vikubwa na vya kati na vidogo.

Alisema kwa mujibu wa sheria hiyo, viwanda vikubwa na vya kati vinapewa leseni wakati vile vidogo vinapewa usajili.

Mkapa alisema ada ya leseni na usajili inalipwa mara moja na kwamba mmiliki hatozwi tena kwa muda wote wa uwekezaji.

Alisema tozo za BRELA kwa viwanda vyenye mtaji usiozidi Sh. milioni tano ni Sh. 10,000 wakati mtaji usiozidi Sh. milioni 10 ni Sh. 50,000.

"Cheti cha usajili kwa viwanda vidogo vyenye mtaji usiozidi Sh. milioni 100, ni cha kudumu na kinalipiwa mara moja tu... kadhalika viwanda vikubwa vyenye mtaji unaozidi kiasi hicho vinalipia leseni ambayo ni Sh. 800,000 nayo inalipwa mara moja pekee," alisema.

Mkapa alisema kuwa baada ya kusajiliwa na kupewa leseni, wenye viwanda wanapaswa kuwasilisha taarifa kwa msajili kila mwaka bila gharama.

"Uhusiano na mikataba ya kimataifa ambao nchi inaingia unafungua masoko kama vile Soko Huru la Biashara Afrika (AfCFTA), soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na kwingineko. Usipojisajili ni vigumu kuwa na vigezo vya kufikia masoko makubwa na kukua," alisema.

Ofisa huyo alisema masharti ya leseni na usajili wa viwanda ni rahisi kwa kuwa hakuna tozo za mwaka; badala yake ni taarifa zinazoainisha changamoto na mafanikio kila mwaka kwa ajili ya serikali kuweka kumbukumbu za huduma na bidhaa zinazozalishwa nchini na kuwezesha kutunga sera nzuri.

Kwa mujibu wa Mkapa, viambatanisho vya kusajili kiwanda ni pamoja na andiko la mradi, uthibitisho wa eneo kilipo na kibali cha Baraza la Taifa la Hifadhi Mazingira (NEMC).

Mkuu wa Kampuni katika Kurugenzi ya Kampuni na Majina ya Biashara BRELA, Lameck Nyangi, aliwataka wavumbuzi kujisajili ili kulinda kazi pamoja na ma-

# Tanesco yajivunia mifumo ya kidijiti

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limesema huduma zake nyingi zinapatikana katika mifumo ya kidijiti hali iliyosaidia kuleta mageuzi makubwa ya utoaji wa huduma.

Uwekezaji huo ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuyataka mashirika ya umma yawekeze katika mifumo hiyo ya kidijiti.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa huduma kwa wateja wa Shirika hilo, Fatuma Mohamed, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika jijini Dodoma.

Alisema uwekezaji uliofanywa na shirika hilo kwenye mifumo ya TEHAMA umesaidia kwa kiwango kikubwa kuleta mageuzi kwenye utoaji wa huduma na kuwapunguzia gharama wateja. Alisema TANESCO ambalo ni shirika la umma limejikita kutoa huduma katika mfumo wa kidijitali kuanzia kuunganisha umeme pamoja na kuongeza wigo katika matumizi ya TEHAMA kwa upande wa kutoa taarifa kwa jamii kuhusu shirika hilo.

"TANESCO limejikita pia katika kutoa huduma katika mfumo wa kidijitali tukianzia na mfumo wetu wa kuunganisha umeme wa NIKONECT, ambao ni wa kidijitali kwa sasa mteja siyo lazima afike ofisini ili kupata huduma ya kuunganishiwa umeme," alisema.

"Mteja popote alipo akiwa na simu janja au hata akiwa na simu zile za kitochi anaweza kufanya maombi na anaweza kuunganishiwa umeme bila kufika ofisi za TANESCO," alisisitiza.

Fatuma alisema shirika hilo limeongeza wigo wa kutumia TEHAMA kwa upande wa kutoa taarifa mbalimbali ambayo unaitwa JISOT na kupitia mfumo huo mteja anaweza akatoa taarifa kwa njia ya simu janja.

"Kwa kupitia namba yetu ile ile ya kutolea taarifa kwenye kituo cha miito ya simu TANESCO na kwa kweli tumeona mafanikio makubwa kwani wananchi wanahudumiwa kwa haraka wanapotoa taarifa zao," alisema.

Alisema kwa kutumia JISOT taarifa hiyo inatumwa kupitia namba ya kutolea taarifa kwenye kituo cha miito ya simu Tanzania TANESCO ambayo namba hiyo pia inatumika kwa mtandao wa kijamii.

Aidha, alisema faida ya huduma hizo ni kuokoa muda wa mteja kusafiri umbali mrefu pamoja na usumbufu wa kutafuta ofisi, ili kujipatia huduma, lakini pia TANESCO wameweza kupata taarifa kwa haraka kiganjani na urahisi wa kuhudumia wateja kwa uharaka.

Fatuma alisema mfumo wa JISOT unamruhusu mteja kujihudumia mwenyewe kwa kuuliza maswali au kupitia changamoto atakazozipata kutokana na huduma au hitilafu ya umeme itakayojitokeza kwenye eneo lake.


halopesa

THE REGISTERED TRUSTEES OF HALOPESA
FINANCIAL STATEMENTS FOR THE PERIOD ENDED 31 DECEMBER 2023

STATEMENT OF COMPREHENSIVE INCOME

| | NOTE | 2023 (TZS) | 2022 (TZS) |
|---|---|---|---|
| Operating expenses | 6 | (19,719,264) | (19,252,292.00) |
| Operating loss | | (19,719,264) | (19,252,292.00) |
| Finance income | 7 | 4,077,451,943 | 3,150,701,194.00 |
| Finance costs | 7 | (3,653,388,279) | (2,843,996,200.00) |
| **Profit before tax** | | **404,344,400** | **287,452,702.00** |
| Income tax expense | 8 | (404,344,400) | (287,452,702.00) |
| **Loss for the year/period** | | — | — |
| Other comprehensive income | | — | — |
| **Total comprehensive income for the year/period, net of tax** | | — | — |

STATEMENT OF FINANCIAL POSITION

| ASSETS | NOTE | 2023 (TZS) | 2022 (TZS) |
|---|---|---|---|
| **Current Assets** | | | |
| Cash and bank balances | 9 | 110,959,347,606 | 114,400,588,199 |
| **TOTAL ASSETS** | | **110,959,347,606** | **114,400,588,199** |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | | |
| **Equity** | | | |
| Accumulated profit | | — | — |
| **Current liabilities** | | | |
| Amounts due to customers | 10 | 110,947,443,606 | 114,388,934,749 |
| Other liabilities | 11 | 11,904,000 | 11,653,450 |
| | | **110,959,347,606** | **114,400,588,199** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | | **110,959,347,606** | **114,400,588,199** |

STATEMENT OF CASH FLOWS

| | NOTE | 2023 (TZS) | 2022 (TZS) |
|---|---|---|---|
| **Operating activities** | | | |
| Profit before tax | 8 | 404,344,400 | 287,452,702 |
| **Working capital changes** | | | |
| Increase in amounts due to clients | | (3,441,491,143) | 47,398,212,104 |
| Increase in other liabilities | | 250,550 | (22,977,056) |
| Increase in restricted bank balances | | 3,441,240,593 | (47,375,235,048) |
| Income tax paid | | (404,344,400) | (287,452,702) |
| **Net cash flows used in operating activities** | | — | — |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | | — | — |
| Cash and cash equivalents at beginning of the year/period | | — | — |
| **Cash and cash equivalentsat 31 December** | 9 | — | — |

HABARI KITAIFA

# Ummy azindua kampuni tanzu ya Bohari ya Dawa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu amezindua Kampuni Tanzu ya Bohari ya Dawa (MSD MEDIPHAM Manufacturing Co. Ltd), itakayosimamia viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya, pamoja na kuzindua Bodi ya Usimamizi wa kampuni hiyo.

Aliisisitiza kampuni hiyo kushirikisha wabia watakaokuwa tayari kushirikiana na MEDIPHAM kuzalisha bidhaa za afya, na kuendelea kutoa kipaumbele wazalishaji wa ndani.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya MSD, Rosemary Silaa, alisema kuwa kuwa kampuni hiyo ni matokeo ya Sheria ya MSD kufanyiwa marekebisho mwaka 2021, na kuongezewa jukumu la kuzalisha bidhaa za afya na amewaelekeza wajumbe hao wa bodi kuandaa mpango mkakati wa kampuni hiyo, pamoja na mfumo wa kutathimini namna ya kufikia malengo watakayojiwekea.

Silaa alisema ana imani kuwa kampuni hiyo itafanikiwa, ikiwa na mikakati mizuri, akitoa mfano kuwa kiwanda cha barakoa kilianza mwaka 2021 na mtaji wa Sh. bilioni 1.6 na hadi sasa wameshapata faida ya Sh. bilioni 4.8. Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, amesema tayari kuna viwanda vitatu vinavyozalisha, ambavyo ni pamoja na viwili vya barakoa (surgical& N95) vilivyopo Keko na kiwanda cha mipira ya mikono cha Idofi, Makambako.

Viwanda vingine vilivyopo mbioni kuanzishwa, ni pamoja na cha dawa Zegereni, Kibaha na cha bidhaa za pamba mkoani Simiyu. Tukai, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya usimamizi wa Kampuni Tanzu (MSD MEDIPHAM), alisema kuwa jukumu lao kubwa ni kuhakikisha miradi yote iliyoanzishwa inaendelezwa na uendeshaji wake kuwa wenye tija.



Mafundi wa mkandarasi wakiendelea na maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi ya mwendokasi katika Mtaa wa Ohio, katikati ya Jiji la Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Rais Guinea Bissau kuzuru nchini siku tatu, kutembelea SGR

**Na Christina Mwakangale**

RAIS wa Guinea Bissau, Umaro Sissoco Embalo, anatarajiwa kufanya ziara ya siku tatu nchini leo, huku akitarajia kutembelea mradi wa treni ya kisasa (SGR).

Kadhalika, nchi hiyo ambayo imefanikiwa katika biashara ya korosho kuuza nje ya nchi kwa asilimia 90, ujio wa rais huyo pia utatoa uzoefu wa namna walivyofanikiwa kwenye zao hilo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Dk. Samwel Shelukindo, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salam jana, alisema ujio huo utaimarisha uhusiano na biashara.

"Urari wa kibiashara hauko vizuri sana, kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 urari wa biashara haukuzidi dola 200,000 hivyo mkakati utakaoanzishwa utakuza biashara, kwa wananchi wetu kupeleka kule bidhaa," alisema Dk. Shelukindo.

Alisema baada ya kuwasili nchini atapokewa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na Waziri January Makamba, na baadaye Ikulu na mwenyeji wake Rais Samia Suluhu Hassan.

"Ingawa kipaumbele pia ni katika kukuza biashara kwenye zao la korosho, wao wamefanikiwa katika zao hili, ili tujifunze, ushirikiano katika uzalishaji wa zao la korosho."

Balozi Dk. Shelukindo aliongeza kwamba pia ajenda zingine ni pamoja na masuala yanayohusu udhibiti wa ugonjwa wa malaria kupitia Taasisi ya Muungano wa Viongozi wa Afrika katika Kudhibiti Malaria (ALMA) na ushirikiano katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Alisema Rais Embaló, ambaye pia ni Mwenyekiti wa ALMA, atafafanua ziara kwenye ofisi za taasisi hiyo zilizopo nchini, ili kupanga mikakati ya kupanua wigo wa taasisi, ambayo ilianzishwa mwaka 2009 na viongozi wa nchi 55 za Afrika, kwa lengo la kutokomeza ugonjwa huo, ifikapo mwaka 2030.

"Tanzania na Guinea Bissau, zimedhamiria kuimarisha na kuinua kiwango cha ufanyaji biashara na uwekezaji hususan kupitia Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA), nchi zote mbili zimeridhia uanzishwaji wa eneo hilo.

"Itakumbukwa wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika mwaka 2023, Mwenyeki, Rais Embaló alizitambua nchi sana, ikiwamo Tanzania kwa kubuni matumizi bora ya Kadi ya Alama ya ALMA (ALMA Scorecard) inayosisitiza uwajibikaji.

Akizungumzia kuhusu uzalishaji wa zao la korosho, alisema Guinea Bissau imejikita katika uzalishaji wa zao hilo ambalo nchi hiyo huuza zaidi nchini India.

"Thamani ya uuzaji nje wa zao hilo inafikia takribani asilimia 90 pia zao hilo ni chanzo kikuu cha mapato kwa wakulima wadogo wa nchi hiyo, kwa asilimia 80 na huchangia asilimia 10 ya Pato la Taifa la Guinea Bissau.

"Inatarajiwa kupitia ziara hii, suala la uzalishaji wa zao la korosho ambalo pia hulimwa hapa nchini, hususan katika mikoa ya Kusini ikiwamo Mtwara na Lindi, litajadiliwa kwa kina," alisema Balozi huyo.

Pia, alisema Rais Embaló na ujumbe wake watatembelea Miundombinu ya Reli ya Kisasa katika Kituo cha Stesheni, jijini Dar es Salaam na Mamlaka ya Eneo Huru la Uwekezaji kwa Mauzo Nje (EPZA).

# Wakulima wa miwa kunufaika upanuzi wa kiwanda

**Na Mwandishi Wetu,** KILOMBERO

WAKULIMA wa miwa wanatarajiwa kunufaika na upanuzi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero.

Baada ya kukumbwa na changamoto za msimu uliopita zilizosababishwa na mvua kubwa ya El Nino, kiwanda hicho kimechukua hatua kuwatuliza na kuwafariji wakulima kupitia mradi wa upanuzi wa kiwanda cha K4 ambao umefikia asilimia 90.

Ni uwekezaji unaofanywa na kampuni kwa kuonesha imani yake kwa jamii ya wakulima wa ndani, ambao watazalisha asilimia 60 ya miwa inayohitajika katika kiwanda hicho.

Pierre Redinger, Mkurugenzi wa uzalishaji wa kilimo wa kampuni hiyo, alisema jana kuwa katika mashamba ya miwa kuwa, "safari hii ilianza mwaka 2018 kwa usajili wa wakulima, ikiungwa mkono na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, ambayo ilifungua njia kwa biashara hii muhimu."

Redinger pia alitangaza kuwa Kampuni ya Kilombero Sugar imejitolea kutoa mkopo wa mbegu za miwa tani 20,000 kwa wakulima, kwa msimu wa upandaji wa 2024/25 na 2025/26, ambao utasaidia zaidi upanuzi huo.

George Gowelle, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari Tanzania, alieleza mchango wa serikali katika mradi huo, akisema kuwa serikali itaendelea kuunga mkono juhudi zinazolenga kuongeza utoshelevu wa sukari.

Alisema, "Kilombero Sugar imeweka mfano wa kuigwa, na serikali itaendelea kuunga mkono jitihada kama hizi."

Bakari Mkangama, Mwenyekiti wa Kilombero Joint Enterprises Cooperatives Society, inayowakilisha AMCOS 17 zinazofanya kazi moja kwa moja na Kampuni ya Kilombero Sugar, alisifu hatua hiyo kama fursa ya mabadiliko.

"Mpango huu utaleta mabadiliko makubwa kwa soko letu la kuaminika, kipato endelevu na kuboresha maisha. Tunapaswa kuchangamkia fursa hii adhimu," alisema.

Mgeni Rasmi, Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dunstan Kyobya, alipongeza juhudi za Kilombero Sugar, akisema upanuzi wa kiwanda cha K4 na kampeni ya kuinua wakulima ni jambo muhimu kwa kipato endelevu kitakachoboresha maisha ya wakulima wa miwa katika Bonde la Kilombero.

"Serikali imejitolea kuunda mazingira mazuri kwa uwekezaji wa biashara na ustawi wa jamii," alisema Mkuu wa Wilaya.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali ilipe wazabuni wake kwa wakati kuepuka hasara

**KATIKA** toleo letu la jana, tulikuwa na habari kuhusu serikali kuuziwa bidhaa na huduma kwa bei kubwa kuliko iliyoko sokoni.

Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) wa zamani, Ludovick Utouh alisema hali hiyo inachangiwa na tabia iliyoko serikalini ya kuchelewesha malipo kwa wazabuni.

Kwa mujibu wa Utouh, hivi sasa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, wazabuni hulazimika kuweka bei kubwa kuliko ya bei ya sokoni wanapoomba zabuni serikalini kwa kuwa serikali hawana uhakika wa kulipwa kwa wakati.

Utouh aliyekuwa CAG nchini kwa miaka minane kuanzia 2006 hadi 2014, alisema kuwa mzabuni hulazimika kuiuzia serikali bidhaa au huduma kwa bei kubwa ili kulinda thamani ya fedha pale malipo yake yatakapocheleweshwa.

Kukiwa na angalizo hilo la CAG mstaafu, Januari 30, mwaka huu, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba alitoa taarifa bungeni kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi Desemba 2023, serikali ililipa wazabuni na makandarasi wa ndani zaidi ya Sh. trilioni 2.1 kati ya madai ya zaidi ya Sh. trilioni 3.1 yaliyowasilishwa.

Alisema kuwa madeni ya Sh. bilioni 981.79 yalikataliwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kukosekana kwa nyaraka, madeni kubainika kulipwa tayari pamoja na makosa ya ukokotoaji.

Kwa mujibu wa waziri huyo, serikali imeongeza bajeti ya kulipa madeni kutoka wastani wa Sh. bilioni 400 hadi Sh. bilioni 700 kwa mwaka na kuahidi kuwa madai ya wazabuni na makandarasi yataendelea kulipwa kadri watakavyowasilisha hati zao za kukamilisha kazi.

Hata hivyo, Nipashe tunafahamu kwamba ucheleweshaji malipo ya wazabuni na makandarasi unakiuka sheria za nchi. Kifungu cha 44(1) cha Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kinaelekeza kwamba, ili kuzisaidia kampuni za ndani na kuziwezesha kutekeleza majukumu yao ya mkataba, taasisi nunuzi lazima zihakikishe malipo yanafanyika kwa wakati kwa wazabuni.

Vilevile, inaporejewa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2022/23, inaeleza kuwa baada ya kukagua na kuthibitisha taarifa za kifedha za wizara, idara zinazojitegemea, na wakala za serikali, alibaini kuwapo madeni ambayo hayakulipwa yenye thamani ya Sh. trilioni 3.39 kufikia tarehe 30 Juni 2023 katika taasisi 20.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 228.16 (asilimia saba) zilikuwa madai ya wafanyakazi; Sh. trilioni 1.37 (asilimia 40) zilikuwa madeni ya wazabuni; na Sh. trilioni 1.79 (asilimia 53) zilikuwa madeni mengine.

Madeni yenye thamani ya Sh. trilioni 1.88 (asilimia 56 ya madeni yote) ni ya muda mrefu, yakiwa yamelimbikizwa kwa zaidi ya miezi 12 na madeni yenye thamani ya Sh. trilioni 1.51 (asilimia 44) ni ya kipindi cha chini ya miezi 12.

Ni takwimu zinaonesha kuwapo umuhimu wa kuweka jitihada zaidi ili kuzuia madeni ya aina hii kuongezeka zaidi serikalini na kuchochea wazabuni kuizuia bidhaa na huduma serikali kwa bei kubwa zaidi ya soko kama ilivyofafanuliwa na CAG mstaafu Utouh.

Tukitambua athari za wazabuni kuizuia serikali huduma na bidhaa kwa bei ghali, tunashauri taasisi nunuzi kulipa wazabuni na makandarasi kwa wakati. Utaratibu uliopo unaongeza mzigo kwa serikali - malipo ya ziada kwa wazabuni yangetumika kutekeleza miradi au kutoa huduma muhimu kwa wananchi.


Tunakumbusha pia taasisi za serikali kuwa Kanuni E. 23 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 inataka madai ya wafanyakazi kulipwa wakati yanapojitokeza.


Hivyo, ni muhimu serikali (Wizara ya Fedha) na taasisi nunuzi watoe kipaumbele katika utoaji fedha kwa ajili ya kulipa madeni ili kupunguza hatari zinazoweza kutokea kwa kuchelewesha malipo, ikiwamo wazabuni kuizuia serikali huduma kwa bei ghali zaidi ya soko.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Urasimu ardhi na maeneo haya.... kwa wawekezaji, maboresho lazima

Na Joyce Lameck

**UWEKEZAJI** katika nchi, ni jambo linalokuza uchumi na kuongeza fursa kwa watu katika kupata ajira. Tanzania sasa imejikita katika uwekezaji wa viwanda mbalimbali, ili kuwa na ubunifu kwa watu wengi nchini.

Sekta ya viwanda ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwa ujumla. Inachangia kuongezeka uzalishaji, uwekezaji usiobadilika, mauzo ya nje, ajira, na utumiaji wa uwezo.

Maendeleo ya viwanda yanaangaziwa kuwa muhimu kimkakati, kwa maendeleo ya jumla ya uchumi wa nchi

Fursa mbalimbali hutokea pale wawekezaji wanapokuwa wametoa nafasi za ajira kwa wenyeji wa eneo hilo na kuwawekea nafasi nzuri ya kiuchumi wao binafsi na kwa taifa kwa ujumla, viwanda hubeba kundi la watu na kuwapa nafasi. Unajenga msingi shindani na endelevu wa viwanda wenye kuwezesha biashara ulimwenguni, kwa kuzingatia faida za mahali tulipo kijiografia na rasilimali zilizopo nchini kupitia sera, mikakati na mipango kwa mageuzi shirikishi ya viwanda.

Uhamasishaji kwa wawekezaji kuja Tanzania, ambako kuna fursa nyingi, ikiwamo Maliasili na Utalii, Kilimo, Madini, na utalii wa fukwe, pia kuna maeneo mengi ambayo bado yana nafasi ya kujenga viwanda kwa wawekezaji.

Pamoja na jitihada za serikali kuhamasisha wawekezaji kuja kuwekeza nchini, bado zipo changamoto zinazowakabili wawekezaji, ili kupata umiliki halali wa maeneo kwa ajili ya kujenga majengo ya viwanda mbalimbali hapa nchini. Bado serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara nchini, ikiwamo kuanzisha mfumo wa dirisha moja la huduma kwa wawekezaji, ili kurahisisha huduma ya usajili na upatikanaji vibali kwa wakati mmoja.

Aidha, hadi sasa Serikali ya Awamu ya Sita, imeweka jitihada zaidi na msukumo katika kurejesha na kuendeleza mahusiano ya kiinchi na nchi, kikanda na jumuiya ya kimataifa, hii inahusisha pia vyombo vya udhamini uwekezaji na utatuzi wa migogoro.

Serikali ipo kwenye hatua ya kuhakikisha kuwa hatua kubwa za kimageuzi katika sheria na uendeshaji, ili kuifanya Tanzania moja ya sehemu sahihi kuwekeza katika nyanda tofauti kwenye kanda.

Mageuzi hayo yanahusisha maeneo mbalimbali, yakiwamo mfumo wa kodi, kuunganisha mifumo na kuondokana na matumizi ya makaratasi, kuunganisha taasisi, Sheria za Ardhi, ili kuondoa vikwazo vya kukuza uwekezaji wa viwanda nchini.

Wawekezaji wa kigeni wanaweza kupata ardhi kwa ajili ya uwekezaji kupitia uwekezaji Tanzania, ambapo anapewa haki ya matumizi ya ardhi, pia kuna njia mbili za kupata ardhi kwa ajili ya uwekezaji ambao serikali imetoa kibali kutumika.

Mwekezaji anapaswa kuomba kutwaa ardhi kutoa katika kijiji halafu na kufuata hatua zote zinazotakiwa mpaka ardhi iidhinishwe kutoka katika ardhi ya kijiji na kuwa ya jumla na kukabidhiwa Tume ya Taifa ya Uwekezaji (TIC) ili kutayarisha haki ya matumizi ya ardhi kwa wawekezaji.

Aidha, mwekezaji anaweza kununua ardhi kwa mtu au kampuni ikiwa ni baada ya mnunuzi na muuzaji kukubaliana kuhusu bei, muuzaji anatakiwa kukabidhi hati miliki ya ardhi kwa kamishna wa ardhi ili aweze kutoa upya hati hiyo kwa jina la TIC na mwishoni atatayarisha haki ya matumizi ya ardhi kwa mwekezaji. Kumekuwapo mchakato mrefu wa kupata kibali na miliki ya kujenga majengo ya viwanda nchini, hata kusababisha wawekezaji kukosa uhalali kwa wakati kufanya mchakato wa kupata ardhi mapema na kuanza jukumu la ujenzi mara moja.

Ni vema njia za kufanya mwekezaji kupata ardhi lipewe kipaumbele, ili kuweka wepesi kwa kupata ardhi kiurahisi na kuwezesha kuanza kazi kwa haraka itasaidia kuvutia wawekezaji mbalimbali kutoka nchi nyingine kuja kuwekeza Tanzania, kutokana na mchakato kuboreshwa.

Pia, kuna changamoto ya kodi kuwa juu, kupelekea wawekezaji walio wengi kushindwa kumudu na kuachana na suala la kuwekeza nchini, kutokana na gharama kama serikali inapaswa kuangalia suala hili kwa upya ili kurahisisha fursa ya uwekezaji kwa mataifa mengine. Kwa kutazama hayo, changamoto hizo na zikafanyiwa kazi, itasaidia kuwavutia na kushawishi wawekezeji kuja kuwekeza Tanzania, kupitia sekta mbalimbali kama vile kilimo, madini, uzalishaji wa vitu ambavyo vimekuwa vikisafirishwa kutoka nchi za nje.

HABARI KITAIFA

# Wanahabari watoka na maazimio sita kongamano la maendeleo sekta yao

Na Jenifer Gilla

WASHIRIKI wa Kongamano la Pili la Maendeleo ya Sekta ya Habari wameazimia mambo sita, ikiwamo vyombo vya habari kuhakikisha vinakuwa na vyanzo mbadala vya mapato ili kulinda na kuendeleza uchumi wao kuliko kutegemea matangazo pekee.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari - Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Thobias Makoba, alieleza maazimio hayo wakati akifunga kongamano hilo jijini Dar es Salaam juzi.

Alisema washiriki wa kongamano hilo pia wameridhia wizara na taasisi za serikali zinazodaiwa na vyombo vya habari nchini kuhakiki na kuweka utaratibu wa kulipa madeni hayo kabla ya Decemba 2024 kama ilivyoagizwa na Rais Samia Suluhu Hassan

Makoba pia alisema washiriki wameridhia agizo la Rais kuwa madeni hayo yakilipwa, wamiliki wa vyombo hivyo nao wawalipe waandishi wa habari mishahara na stahiki zao nyingine pamoja na kuwapa mikataba ya ajira waandishi ambao hivi sasa hawana.

Alisema washiriki hao pia wamekubaliana kuomba serikali kuangalia namna ya kurekebisha sheria katika uwekezaji wa vyombo vya habari ili kutoka umiliki wa asilimia 46 ya sasa kwa wageni hadi 75 ili kuvutia mitaji kutoka nje kunusuru uchumi wake.

"Alisema azimio la tatu ni serikali irekebishe vifungu 12 ambavyo havijarekebishwa katika Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 iliyopitishwa na Bunge mwaka jana," alisema.

Makoba alisema washiriki waliazimia vyombo vya habari viandike maudhui yenye kujenga umoja, kuleta amani na kutetea nchi dhidi ya propaganda zinazolenga kuchafua nchi na vyombo vya habari vya kijamii kuandika miradi inayotekelezwa na serikali katika maeneo hayo.

Washiriki pia wameazimia kuwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani, vyombo vyote vya habari vitoe fursa sawa kwa vyama vyote vya siasa.

Vilevile, wamekubaliana vyombo vya habari vya mitandaoni viongeze ubunifu na kuandaa maudhui yenye tija na kuongeza uaminifu kwa walaji.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye alisema ameyapokea maazimio hayo na atakwenda kuyafanyia kazi, huku akisisitiza kuwa hoja ambazo hazijafanyiwa kazi katika maboresho ya Sheria ya Huduma za Habari walishajadili kwanini hazitofanyiwa kazi.

Alisema mada hizo ziendelee kuleta mageuzi na chachu katika maendeleo ya sekta hiyo, ikiwamo kuleta ushirikiano katika serikali na ushindani kwa nia ya kujenga nchi. Alisema atatengeneza sekta ya habari vizuri ili inufaishe waandishi wa habari wa sasa na vizazi vijavyo, akiomba wamwamini kwa kuwa hatowaangusha.



Msemaji Mkuu wa Serikali, Thobias Makoba.

"Niwahakikishieni tutakwenda hatua kwa hatua, yanayowezekana tutayafanya na yasiyowezekana yatafanyika kwa wakati sahihi kwa sababu siwezi kwenda kinyume cha sera," alisema Nape.

Waziri huyo alisema kongamano hilo limeiunganisha waandishi wa habari wote wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na limechangia kuboresha ukuaji wa sekta na ombi lake ni nguvu ya kujadiliana iendelee na ipelekwe hadi kwa Watanzania ili wapende kujadili mambo ya nchi yao.

Aliagiza waandishi wa habari kutengeneza majukwaa ya kuwaweka viongozi wa nchi ili waongelee masuala yanayolenga kujenga nchi yao ili kuchochea maendeleo ya nchi.

Alisema waandishi wa habari wakiamua wana uwezo wa kutengeneza wanasiasa ili waelekeze nguvu zao katika kujenga nchi yao.

"Mimi ni mwanasiasa na pia mwandishi wa habari, ninaelewa nguvu tulionayo, tukilitaka jambo letu," Waziri Nape alisema.

Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Nyanda Shuli, alisema waandishi wa habari wana wajibu mkubwa wa kufichua uovu na kurudisha viongozi katika mstari ili wasivuke mipaka ya madaraka walionayo, akionya kuwa waandishi wa habari wakifumbia macho mienendo ya viongozi, wanaweza kuvunja haki za binadamu.

Shuli pia alisema kuna haja kuwa na uhusiano mzuri kati ya vyombo vya habari na maofisa wa habari wa taasisi za serikali ili kufanya kazi ya kuhabarisha umma kwa weledi.

Akichangia mada inayohusu fursa na changamoto za Akili Mnemba, Mkurugenzi wa Usalama wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari katika Wizara ya Habari, Stephen Wangwe, alisema waandishi wa habari nchini wanapaswa kuendana na kasi ya ukuaji wa teknolojia, vinginevyo wataachwa nyuma na wenzao wa mataifa ya nje.

Alisema serikali ina mpango wa kuandaa sera na mikakati ya matumizi ya akili mnemba ili waandishi wa habari wanapoitumia wasitoke nje ya maadili na utamaduni wa nchi yao.

Alisema ili teknolojia hiyo isibadilishe mwenendo wa maudhui yanayoendana na utamaduni wa nchi, kunahitajika wataalamu wabobezi na vitendea kazi vya kisasa kama kompyuta ili kutengeneza hifadhidata yenye taarifa inayoendana na mandhari hayo.

Alisema pia kuna haja ya kuongeza kasi ya kutoa mafunzo ya namna ya kutumia akili mnemba kwa waandishi wa habari ili wanapotengeneza maudhui kwa kutumia teknolojia hiyo wasitoke nje ya maadili ya nchi yao.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (Misa-Tan), Salome Kitomari aliwatoa hofu waandishi wa habari kuwa akili mnemba haitachukua ajira zao kwa kuwa kwenye mchakato wa habari kuna hatua nyingi zitakazomhitaji binadamu ikiwamo kwenda kufanya mahojiano, kurekebisha majina ya maeneo na watu ambayo ni ya Kiafrika - akili hiyo haiwezi kuyatambua kwa mfumo wa mashine.

Salome ambaye pia ni Mhariri wa Habari wa Gazeti Nipashe, alisisitiza umuhimu wa waandishi wa habari kujifunza matumizi sahihi ya teknolojia hiyo ili wasifanye makosa ambayo yanaweza kuwagharimu katika ajira zao na kutumia fursa lukuki zilizoletwa na akili mnemba ambazo zinarahisisha na kuharakisha mchakato wa upashanaji habari.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, alikumbusha waandishi wa habari kufuata sheria na taratibu zinazowaongoza wakati wanatekeleza majukumu yao ili kuepuka kuingia katika mikono ya sheria.

Awali Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa Benki ya NMB, Alfred Shao, alipongeza serikali kwa mapinduzi chanya kwenye sekta ya habari, huku ikikiri kuvutiwa na mchango wa vyombo vya habari katika kustawisha uchumi endelevu kupitia huduma jumuishi za kifedha kwa wananchi.

Shao alisema sekta ya fedha, hasa benki yao, inatambua na kuthamini mchango wa serikali kupitia Wizara ya Habari pamoja na vyombo vya habari katika kuchochea huduma jumuishi kwa wananchi.

"Tunaipongeza serikali kwa ongezeko kubwa la vyombo vya habari lililochangiwa na kuimarishwa kwa sekta ya habari, ongezeko linaloakisi uhuru wa habari ulioiwezesha Tanzania kutajwa kama kinara wa uhuru huo kwa nchi za Afrika Mashariki," alisema.

Shao alisema benki hiyo ni mdau mkubwa katika kukuza uchumi endelevu na wanaamini kwa kushirikiana na vyombo vya habari, wana uwezo mkubwa wao na taasisi zingine za fedha kufikia wananchi kwa uharaka, urahisi na wepesi na kuwajumuisha katika mnyororo huo.

Kongamano hilo la siku mbili na kikao kazi cha siku nne lilifunguliwa Jumanne na Rais Samia likiwa na kaulimbiu ya 'Jenga Mustakabali wa Endelevu Kwenye Sekta ya Habari Katika Zama za Kidijiti'.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



## HABARI KITAIFA



Msamaria mwema akisaidia kumvusha mwanamke kwenye maji yaliyojaa katika Mtaa wa Pamba, jijini Dar es Salaam jana, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha. **PICHA: JOHN BADI**

# Kipindupindu chaua wawili Lupaso

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WATU wawili wamefariki dunia kufuatia kuwapo mlipuko wa ugonjwa wa kuharisha na kutapika (kipindupindu) katika Kitongoji cha Miesi, Kijiji cha Mbangala, Kata ya Lupaso, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Mtwara huku chanzo kikielezwa kuwa ni ukosefu wa maji safi na salama.

Akithibitisha kutokea kwa vifo hivyo jana wilayani Masasi wakati akitoa taarifa ya kuwapo mlipuko wa ugonjwa huo katika kikao cha dharura kilichoitishwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Lauter Kanoni, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Masasi, Dk. Ruben Mwakilima alisema Idara ya Afya katika hospitali hiyo imethibitisha kuwapo mlipuko wa ugonjwa huo katika kitongoji tajwa.

Dk. Mwakalima alisema watu 47 wameugua ugonjwa huo (wanaume 22 na wanawake 25) na wamefikishwa katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya kupata matibabu.

Alisema kuwa kati ya wagonjwa hao 47, watoto walio chini ya umri wa miaka mitano ni saba, watoto wenye umri wa miaka mitano hadi 15 ni watano, miaka 15-49 ni wagonjwa 32 na watatu wenye umri wa kuanzia miaka 50.

"Kufuatia mlipuko wa ugonjwa huu wa kuhara na kutapika, wagonjwa wawili (mwanaume na mwanamke) wamepoteza maisha kutokana na mlipuko huu," alisema Dkt. Mwakilima.

Dk. alisema kuwa tarehe 11 Juni 2024, katika Kituo cha Afya Chiungutwa walipokewa wagonjwa watatu wenye dalili za kuharisha na kutapika na sampuli zao zilipochukuliwa na kupimwa katika Maabara ya Ndanda, zilibainika kuwa na vibrio cholerae, vimelea vinavyosababisha ugonjwa wa kipindupindu.

Aliongeza kuwa pamoja na hayo, zipo hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa Ili kudhibiti mlipuko huo ikiwa ni pamoja na kukutana na uongozi wa kijiji na kata kwa ajili ya kuelimisha na kukumbusha majukumu yao wakati wa mlipuko pamoja na kuwafahamisha kuwapo kambi ya matibabu ya wagonjwa wa kuharisha na kutapika katika Kitongoji cha Miesi.

Akisoma taarifa katika kikao cha dharura kilichoitishwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Masasi, Ofisa Afya na Mazingira wa Halmashauri hiyo, Said Ame alisema mnamo Juni 10, 2024, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ilipokea taarifa kutoka kwa Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Utimbe kuhusu kuwapo wa mlipuko wa ugonjwa wa kuharisha na kutapika katika Kijiji cha Mbangala, Kitongoji cha Miesi.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa hiyo, Timu ya Dharura ya Haraka (RRT), ikiongozwa na Ofisa Afya na Mazingira, Daktari wa Hospitali ya Halmashauri na Mtaalamu kutoka RUWASA walitembelea eneo la tukio na kuchukua sampuli ya maji yanayotumika (ya Mto Miesi) kwa ajili ya kufanyia vipimo vya maabara.

Ame alisema maiti zilizokuwa katika Kituo cha Afya Chiungutwa, vipimo vilithibitisha zina vijidudu vya vibrio cholerae.

"Elimu juu ya afya ya kujikinga dhidi ya magonjwa ya mlipuko imetolewa kwenye mkutano wa kijiji, maeneo yenye mkusanyiko, maeneo ya huduma za vyakula na ngazi ya kaya katika Kijiji cha Mbangala," alisema Dk. Ame.

Alisema ugawaji vidonge 1,580 vya kuua wadudu katika maji kwenye kaya 193 za kijiji kilichoathirika umefanyika, kila kaya ikipatiwa vidonge viwili.

Alisema uhamasishaji wa jamii kuhusu ujenzi wa vyoo pia umefanyika, ilani ikitolewa kila kaya kuwa na choo kufikia jana. Kwa kushirikiana na RUWASA, lita 20,000 za maji safi zilisambazwa kijijini huko. Dk. Ame alisema timu pia imetembelea vituo vilivyopata wagonjwa wa kipindupindu na kuelekeza kuchukua tahadhari wakati wa mlipuko na taratibu zingine ikiwamo usambazaji dawa za utakasaji na kutoa maelekezo ya matumizi ya dawa hizo.

Alisema wamefunga vilabu vya pombe za kienyeji kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Lauteri Kanoni alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, kuendelea kutoa taarifa katika vijiji na kata zote kuhusu mlipuko huo ili wananchi wapate taarifa na wachukue tahadhari.

"Wananchi wanapaswa kufahamu kuhusu njia za kujikinga, uongozi wa kijiji uweke ulinzi kwenye milango ya kuingilia ndani ya vijiji na ambao wanaotafuta matibabu Utimbe, kwanza waende kupata matibabu kambini badala ya kwenda zahanati moja kwa moja," alielekeza Kanoni

## Wajasiriamali kunufaika bil.11/- zilizotolewa na EU

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Ulaya (EU) umewapa wajasiriamali wa Tanzania Euro milioni nne (Sh. bilioni 11.202) kwa ajili ya kufanikisha miradi mbalimbali ya kiuchumi popote walipo.

Makubaliano ya kutolewa fedha hizo yamefikiwa jijini Dar es Salaam kati ya EU na Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania (FSDT) wakati wa mkutano uliowashirikisha wadau wakiwamo taasisi za fedha, maofisa wa serikali, wajasiriamali na sekta binafsi.

Wakati wa kutia saini mkataba wa makubaliano hayo, Mkuu wa Ushirikiano wa EU, Cedric Mellel, alisema fedha hizo zinatolewa kwa lengo la kunufaisha wajasiriamali wadogo na wa kati; wanawake na vijana.

Alisema wanufaika ni pamoja na walio kwenye sekta za kilimo, uvuvi (uchumi wa bluu), biashara na miradi ya kuhifadhi mazingira.

Dk. Peter Kingu, Mkuu wa Sera, Wajasiriamali na Huduma Jumuishi za Fedha wa FSDT, alisema asilimia 70 ya wanufaika wa fedha hizo watakuwa wanawake wakati vijana ni asilimia 30.

Alisema wanalenga kuwafikia watu 200 na kuwawezesha kuanzisha, kuendeleza miradi na kununua vifaa au vitendea kazi.

Aliongeza kuwa msaada huo kwa walengwa utaanzia Sh. milioni tano hadi milioni 30 na vitendea kazi vitakavyopata fedha hizo ni vile vinavyopunguza uharibifu wa mazingira.

Dk. Kingu alisema ni pamoja na majiko banifu, yanayotumia nishati jua, pikipiki zinazotumia gesi au betrii na vingine vinavyopunguza uzalishaji hewa ukaa na kuchafua mazingira.

Aliongeza kuwa fedha hizo si mikopo bali ni msaada kwa ajili ya kuendeleza ujasiriamali kwenye sekta mbalimbali kuanzia kilimo, viwanda vidogo, usindikaji, uvuvi na biashara ndogo.

Alisema zitapatikana kwa kuandika andiko la mradi linaloeleweka na lenye kukidhi viwango na sifa za kupewa fedha hizo.

Kamishna wa Kuendeleza Fedha na Uchumi Wizara ya Fedha, Dk. Charles Mwamwaja, alisema ni EU mmoja wa wadau na mshirika wa Tanzania katika kuchangia fedha za maendeleo na safari hii imetoa Euro milioni nne kukuza wajasiriamali wadogo na wakati hasa wanawake.

Alisema benki mbalimbali na taasisi nchini zimepokea fedha kwa ajili ya kutoa mikopo nafuu ya kusaidia wakulima, wafugaji, viwanda vidogo na wavuvi kwenye uchumi wa bluu, ikilenga kuinua wanawake na vijana.

Dk. Mwamwaja alisema fedha hazitolewi bila kukidhi viwango ikiwa ni pamoja na kuandika andiko la biashara lenye sifa na linalokopesheka.

Alitahadharisha kuwa miradi mingi inasuasua kutokana na sababu kadhaa, kubwa zaidi ni kukosa elimu kuhusu fedha, kuweka rekodi, kutunza akiba, ujuzi wa ujasiriamali na elimu ya utafutaji.

Kamishana wa Kuendeleza Fedha na Uchumi, alisema ili kukabiliana na upungufu huo, benki na taasisi nyingine zinawajengea uwezo wanufaika ili miradi iwe endelevu.

Washiriki wa mkutano huo, zikiwamo taasisi za fedha na benki, walisema wanawake wajasiriamali kwenye kilimo, ufugaji, viwanda vidogo, biashara na uvuvi wamenufaika na mikopo na misaada kutoka EU.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

**TAARIFA KWA UMMA**

**(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni ya 20 (4) ya Kanuni za Mafuta Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Rejareja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo:

**Jina la awali la kituo:** **Halima Samli Selemani T/A, Nakapanya Filling Station**
**Nambari ya Leseni:** **PRL-2021-071**
**Mahali Kituo kilipo:** **Eneo la Nakapanya, Wilaya ya Tunduru, Mkoa wa Ruvuma**
**Jina linalopendekezwa:** **Oilplus Tanzania Limited**
**Mmiliki wa awali:** **Halima Samli Selemani**
**Mmiliki mpya:** **Oilplus Tanzania Limited**

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe ya tangazo hili.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz



# Ummy aonya utumiaji dawa holela

**Na Godfrey Mushi,**
ARUSHA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu amewaonya wananchi kuacha tabia ya kunywa dawa bila uchunguzi wa kitabibu ili kuepuka madhara kiafya.

Kwa mujibu wa Ummy, hali hiyo inaweza kusababishwa na usugu wa vimelea dhidi ya dawa, hasa za antibaotiki kushindwa kufanya kazi, hivyo kugharimu maisha ya watu na nguvu kazi ya taifa.

Akizungumza jijini hapa jana wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Miaka 50 ya Jumuiya ya Afya ya Nchi za Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika (ECSA-HC) alisema kuwa:

"Usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa ni janga kubwa, ambalo jamii inapaswa kupambana nalo kwa dhati, kwa kuwa madhara yake yanagharimu fedha nyingi."

Alisema wananchi wanapaswa kuepuka kutengeneza janga kubwa ambalo litakwenda kuigharimu sekta ya afya kwa siku za baadaye. "Ziko dawa za mifugo anapewa binadamu. Ikiwa umeandikiwa dawa unywe kwa siku tano basi maliza siku zote tano. "Zingatia matumizi sahihi ya dawa, hususani za antibaotiki na usitumie dawa bila ya kuandikiwa na daktari au mtaalam wa mifugo," aliongeza kusema.

Ummy, alisema madhara ya matumizi holela ya dawa hizo, husababisha mgonjwa kukaa hospitalini na kuugua kwa muda mrefu bila kupona. Mengine, ni mgonjwa kutumia gharama kubwa kujiuguza na hata kupoteza maisha kutokana na usugu wa vimelea dhidi ya dawa.

"Kuongezeka kwa mzigo wa magonjwa yasiyoambukiza katika ukanda huu, Jumuiya ya Afya ya Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika (ECSA-HC) imejipanga kuja na tafiti na ushahidi wa kisayansi wa mbinu sahihi za kupambana na magonjwa hayo na kuweka sera nzuri ya afya kwa wote," alisema.

Vilevile, Waziri huyo, alisema miaka 50 ya ECSA-HC ni ya kujivunia kwa kuwa taasisi hiyo, imekuwa ikitoa msaada wa kiufundi katika afya kwa nchi za ukanda wa mashariki, kati na kusini mwa Afrika.



Mratibu wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), mkoa wa Manyara, Malkiadi Mayega (kulia), akitoa mafunzo ya kilimo cha ikolojia kwa wanachama wa mtandao huo na wa Lyamungo Amcos wa kijiji cha Kilanya, Machame Mashariki, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro, hivi karibuni. **PICHA: ZUWENA SHAME**

# 9,000 walipwa fidia ujenzi bomba la mafuta

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

ZAIDI ya wananchi 9,000 wamelipwa fidia kupisha ujenzi wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kuanzia nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Ofisa Mawasiliano ya Umma wa EACOP, Abass Abraham, alisema watu hao ni sawa na asilimia 99.

ECOAP iko Manyara kuelezea ujenzi wa bomba hilo na namna wananchi wanavyonufaika nao.

Abraham, alizitaja kampuni yenye ubia katika mradi huo, kwa ni Total Energies ya Ufaransa, ambayo itakuwa na hisa asilimia 62 na The Uganda National Oil Company (UNOC) 15.

Nyingine ni Tanzania Petrolium Development Corporation (TPDC), asilimia 15 na China National Offshore Oil Corporation (CNOOC) nane.

Alisema watu waliopitiwa na mradi huo walikuwa wanachagua wenyewe kama wanataka kulipwa fidia ya fedha au kujengewa nyumba.

"Na kama mtu alikuwa na nyumba ina vyumba 10 atajengewa, vilevile na tulikuwa tunawajengea nyumba za kisasa," alisema Abraham.

Alisema kwa Tanzania, mradi huo umewajengea watu waliopisha mradi huo nyumba 339 nchi nzima.

Alisema baadhi ya familia ambazo mashamba yao yalichukuliwa kupisha mradi huo ziligawiwa chakula kuanzia miezi sita hadi 12 na kuzipatia elimu ya kilimo ili ziendelee kuwa na uhakika wa chakula. Kuhusu ajira, alisema mkandarasi kijiji ambako kuna mradi huo anapaswa kutoa ajira kwa wananchi wake ili kuondokana na upotoshwaji.Mratibu wa Ushirikishwaji Jamii EACOP Manyara, Emil Msisiri, alisema kwa mkoa huo, vijiji 12 vinapitiwa na mradi huo.

Avijitaja vijiji hivyo na wilaya zake kwenye mabano kuwa ni i Kitwai B (Simanjiro),

Diloda, Gorimba, Gisambalang na Masusu (Hanang') na Mwitikira, Ndorokoni, Ndaleta, Olpapongi, Kemana, Amei na Loolera (Kiteto).

Kwa mujibu wa ofisa huyo, kwa Manyara bomba hilo litapita Hanang' kilometa 17, Kiteto 106 na Simanjiro sita.

Alisema kwa Hanang' walionufaika ni watu 154, Kiteto 313 na Simanjiro 18. Aliendelea kusema kuwa kati ya watu hao waliojengewa nyumba kwa Hanang' 13 ndio na Kiteto 14.

## Waranda mitaani kusaka maji

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKAZI wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga wameomba serikali kuwaondolea kero ya kuranda mitaani na ndoo kusaka maji kwa miaka mingi na kushindwa kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Ombi hilo walilitoa mapema wiki hii wakati wakilalamikia kero hiyo inayoukabili mji wa Muheza.

Mkazi wa Mtaa wa Mdote, Abdallah Mchumiatumbo, alisema wanatumia muda mwingi kusaka maji kwenye visima na mabwawa ambayo si salama kwa matumizi ya binadamu.

Mchumiatumbo, alisema wanalazimika kuchota maji hayo yasiyo salama katika bwala la Muheza Estate na visima vilivyochimbwa kienyeji na baadhi ya wakazi wa mji huo.

Aliishukuru Mamlaka ya Majisafi na Mazingira Tanga (TANGA UWASA) kwa kuwapunguzia kero hilo kwa kupeleka maji ya bomba katika Mtaa wa Mdote.

Hivi karibuni, Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainab Abdallah, aliwatoa hofu wananchi kuwa kero hiyo itabaki historia baada ya Serikali kuanza kutekeleza ujenzi wa mradi wa maji kutoka Mto Pangani hadi mji wa Muheza na kwamba mkandarasi yupo kazini.

## Mamia wamzika ofisa hospitali ya Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

ALIYEKUWA Ofisa Rasilimali Watu wa Hospitali Teule ya Wilaya Muheza mkoani Tanga, Dk. Erick Kombo Sunday amezikwa katika makaburi yaliyopo Kitongoji cha Daisaama Kijiji cha Magila

Dk. Kombo alifariki kwa ajali ya gari iliyotokea mkoani Morogo na maziko hayo kufanyika juzi. Akizungumza katika maziko hayo yaliyohudhuriwa na mamia ya waombolezaji, Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini, Balozi Adadi Rajab licha ya kutoa salamu za pole kwa familia, alisema marehemu huyo ameacha alama ya upendo na Amani kwa jamii.

"Ndugu wafiwa, waombolezaji, kifo hiki kimewagusa wengi kutokana na marehemu alikuwa mtu wa watu. mwenzetu ametangulia, tumwombee kwa yale mazuri aliyofanya wakati wa uhai wake," alisema.

Awali Katibu Mkuu wa Anglikana Dayosisi ya Tanga inayomiliki hospitali hiyo, Charles Mbukuzi, alisema enzi za uhai wake, Dk. Kombo, alitumika kwa uadilifu katika majukumu yake. "Kwa niaba ya Askofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Mahimbo Mndolwa tumepokea msiba huu kwa huzuni, tunatoa pole kwa familia na wafanyakazi wote wa Hospitali ya Mtakatifu Augustino Muheza," alisema Mbukuzi. Christopher Kiango, Kasisi Kiongozi wa Kanisa hilo, Dayosisi ya Tanga katika mahubiri yake, alisema watu wote wanatakiwa kutambua kuwa ni mali ya Mungu.

Kasisi Kiango, alisema ni wajibu wa kila mmoja kutambua kuwa yupo safarini na kwamba wakati na majira yeyote Mungu hujitwalia utukufu.

"Katika hali ya ubinadamu tunasikitika kumkosa ndugu yetu Erick, lakini Mungu hutimiza mapenzi yake kwa mtu yeyote bila kujali umri. Sisi ni mazao shambani mwake, yeye ni mkulima uamua kuvuna zao lolote analopendezwa nalo. Tuendelee kuomba mwisho mwema," alisema.





# Watoto wapaza sauti kwa Samia mwenzao albino aliyeuawa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WATOTO mkoani hapa wamemuomba Rais Samia Suluhu Hassani kuingilia kati kwa kuhakikisha watakaokutwa na hatia ya mauaji ya mtoto mwenzao mwenye ulemavu wa ngozi (albino), Asimwe Novart (2.5) kuhukumiwa kifo ili kukomesha ukatili huo dhidi yao nchini.

Ombi hilo lilitolewa na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Watoto Mkoa wa Shinyanga, Noelina Nicolaus wakati akizungumzia kuhusu kukamatwa kwa watuhumiwa wa mauaji hayo.

Noelina, alisema serikali inapaswa kutoa hukumu kali dhidi ya wataopatikana na hatia ya mauaji hayo kama njia ya kuwasaidia watoto ambao ni nguvu kazi ya Taifa la kesho.

Alisema pia serikali inatakiwa kusimamia kesi za mauaji na ukatili dhidi ya watoto kwa kuwa ni wanyonge, wasiokuwa na nguvu za kujihami wanapovamiwa na watu waovu na kuwateka kisha kuwauwa.

"Tunasikitika na kulaani vikali mauaji ya kikatili ya mtoto mwenzetu Asimwe, tunapata uoga tunaposikia matukio ya kikatili dhidi ya watoto hata watu wazima. Tunaiomba serikali iweke mkazo katika adhabu ya watu wanaotekeleza mauaji yoyote, wauawe haraka kama walivyomuua Asimwe, ikifanya hivyo itasaidia kuondoa ukatili huo," alisema Noelina.

Kwa upande mwingine, aliwataka wazazi kuacha tabia ya ukatili dhidi ya watoto, kuwabagua wenye ulemavu na kutimiza mahitaji yao kwa kuwapatia elimu.

Vilevile, alitoa wito kwa watoto kufuata maadili mema, kuwasikiliza wazazi na kuacha kujiingiza kwenye makundi mabaya na kusababisha mmomonyoko wa maadili miongoni mwao.

Mwenyekiti wa Baraza la Watoto Wilaya ya Shinyanga, Amina Hamis, aliwataka watoto kuacha usiri kwa kukaa kimya wanapofanyiwa vitendo vya ukatili bali wapaze sauti ili wahusika wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Shinyanga, Rehema Edson, aliitaka jamii, mashirika, viongozi wa dini na serikali, kungana kupinga ukatili dhidi ya watoto.

Mkurugenzi wa Shirika la WEADO, Eliasenya Nnko, alisisitiza jamii kuendelea kulinda haki za mtoto na wazazi kuhakikisha watoto wanakua katika makuzi bora.

Nnko, aliiomba serikali kuendelea kuisimamia sheria na kuwachukulia hatua kali watu wanaowafanyia vitendo vya ukatili watoto ili haki itendeke kwa kundi hilo.



Meneja Mkuu wa kampuni ya ununuzi wa zao la pamba ya Nida Textile Kahama, Shahid Hameed akigawa kanga bure kwa wakulima wanawake wa zao la pamba katika kijiji cha Butuyu, kata ya Bunambiyu, Halmashauri ya Kishapu, mkoani Shinyanga, alipowatembelea jana, kusikiliza changamoto zinazowakabili wakati wa mavuno na mauzo sokoni. **PICHA: SHABAN NJIA**

# DC ang'aka madawati kugeuzwa kuni

**Na Rose Jacob, BUNDA**

WAKATI shule za msingi 186 Wilaya ya Bunda Mkoa wa Mara zikikabiliwa na upungufu wa madawati zaidi ya 16,000, mkuu wilaya hiyo, ameng'aka shule moja, madawati yanayohitaji ukarabati mdogo, mbao zake zikitumika kupikia.

Hayo yalibainika wakati Mkuu huyo wa Wilaya hiyo, Dk Vicent Naano akipokea msaada wa madawati 100 kutoka Benki ya NMB kwa ajili ya Shule ya Msingi Bigutu iliyopo Kata ya Bunda Stoo.

Naano alisema akiwa katika ziara yake ya kukagua maendeleo ya sekta ya elimu, kwenye moja ya shule zilizopo wilayani hapa, alikumbana na kisa hicho cha madawati hayo yanayohitaji ukarabati mdogo mbao zake kugeuzwa kuni kwa kupikia.

Naano, alisema baadhi ya watumishi wakiwemo maofisa elimu kata na walimu wakuu, wameshindwa kusimamia madawati yaliyopo yadumu na kutumika kwa muda mrefu na kusababisha yaliyoharibika kugeuzwa kuni badala ya kufanya ukarabati.

"Mkurugenzi nakuagiza kuanzia sasa shule yoyote itakayokuwa na madawati mabovu ofisa elimu wa kata hiyo aondolewe nafasi hiyo kwani hana msaada kwetu, haiwezekani madawati yanaharibika kidogo tu badala ya kufanyiwa ukarabati yanatelekezwa, hii haikubaliki," alionya Naano na kuongeza:

"Kuna shule nilipita wiki iliyopita nikakuta madawati yanatumika kama kuni, ukiangalia ni madawati ambayo yanahitaji ukarabati mdogo tu, lakini kwasababu ya uzembe na kutowajibika kwa wahusika, wameyaacha na kupelekea tatizo la ukosefu wa madawati kuwa mkubwa, " alisema.

Naano, alisema serikali ya wilaya hiyo imekuwa ikifanya jitihada ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wadau ili waweze kuchangia na kuondokana na uhaba huo. Alitaja mkakati mwingine kuwa ni kuwahusisha wazazi ambao wamekubaliana kuungana watatu kutengeneza dawati moja na kulikabidhi shule husika.

Akikabidhi msaada huo, Kaimu Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Dotto Makota, alisema madawati hayo 100 yana thamani ya zaidi ya Sh. milioni12.

Makota, alisema sekta ya elimu ni kipaumbele kwa benki hiyo, kutokana na umuhimu wake kwa maendeleo yake na Taifa na kwamba uboreshaji wa sekta hiyo ni jambo la muhimu kwao. "Serikali yetu inajitahidi kila kukicha kuboresha sekta ya elimu kwa shule za mjini na vijijini, hivyo jitihada hizo zinapaswa kuungwa mkono na wadau wote kufikia malengo ya mazingira bora zaidi ya elimu nchini," alisema.

Alisema kwa miaka saba mfululizo, benki hiyo imekuwa ikitenga asilimia moja ya faida kusaidia sekta za elimu, afya na majanga kwa kuwa ndizo uhai wake.

Diwani wa Kata ya Bunda Stoo, Fravian Nyamigeko, alisema Halmashauri ya Mji wa Bunda inafanya jitihada kuhakikisha wanafunzi wanaondokana na adha ya kukaa chini.

"Wanafunzi wengi bado wanakaa chini na kata yangu ni miongoni mwa kata zenye tatizo hilo kubwa, jitihada zinafanyika kupitia mapato ya ndani na fedha za mfuko wa jimbo kutatua hali hii ili watoto wetu wawe na mazingira bora ya kusomea," alisema Nyamigeko.

Baadhi ya wanafunzi, walishukuru NMB kwa msaada huo kwa kuwa utasaidia kuboresha taaluma shuleni kwao.

"Mbali na kushindwa kuandika vizuri na kutokumuelewa mwalimu, tunapata madhara ya kuugua mafua na nguo kuchafuka kutokana na kukaa chini na mwakati mwingine kwenye vumbi," alisema Anna Samuel, mwanafunzi wa darasa la saba shuleni hapo

# Wakulima kicheko, bei ya pamba yapaa

**Na Shaban Njia,** KISHAPU

KAMPUNI ya ununuzi wa Pamba ya NIDA Textile Co. Ltd wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga imepandisha bei ya kununua zao kwa Sh. 1,320 kwa kilo katika msimu huu wa mavuno ili kuinua uchumi wa mkulima.

Bei hiyo imetangazwa na Meneja Mkuu wa Kampuni hiyo, Shahid Hameed baada ya kutembelea wakulima wa pamba katika Kijiji cha Butuyu Kata ya Bunambiyu wilayani Kishapu na kuwapatia zawadi ya kanga zilizotengenezwa kwa zao hilo.

Hameed alifafanua kuwa kampuni hiyo imepandisha bei ya pamba kwa kuongeza Sh. 170 kwa kilo na kufikia 1,320 kutoka bei elekezi ya serikali 1,150.

Alisema bei hiyo mpya, itakuwa faraja kwa mkulima kumkwamua kiuchumi ambao kwa msimu huu baada ya kilimo hicho kilikumbwa na mvua kubwa.

Alisema kila eneo wanakopita, watanunua pamba kwa bei tofauti na ile elekezi ya serikali.

Alisema uzalishaji wa pamba ukiwa endelevu utasadia kuongezeka kwa bei, kumpa moyo mkulima na kupenda kuwekeza fedha zake katika kilimo cha zao hilo

"Kampuni yetu inategemea wakulima wa pamba, bila wao hakuna NIDA wala uzalishaji wowote unaoweza kufanyika, " alisema Hameed.

Alisema wakulima wengi wamepata elimu ya kilimo cha kisasa na kuzingatia kanuni 10 bora katika kilimo zinazotolewa na maofisa ugani wa kata

Alisema kampuni hiyo inatarajia kupeleka mifuko 500 ya kubebea pamba wakati wa mavuno na mauzo badala ya kutumia kanga, vitenge na kusafirisha kwa mikonoteni kusababisha zao hilo kuchafuka kwa michanga.

Ofisa Kilimo wa Kata ya Bunambiyu, Emmanul John, alisema elimu ya kilimo cha kisasa imekuwa ikitolewa katika mikutano ya hadhara na mkulima mmoja mmoja na kusaidia kuongezeka kwa mavuno ya pamba.

Alisema kata hiyo ina zaidi ya wakulima 3,585,kati ya 1,962 ni wa pamba na 1,623 mazao mchanganyiko.

Agnes Mathias, Mkazi wa Kijiji cha Butuyu, alisema ongezeko la bei kwa Sh 170, limesaidia wakulima wengi kuvuta umeme wa Mamlaka ya Nishati Vijijini (REA) kwenye nyumba zao na kuondokana na matumizi ya vibatari.

Faustine Deusi, alisema amelima hekari 12 za pamba, kati ya hizo, nane kwa kutumia trekta na nyingine ng'ombe.

Ameiomba NIDA kumkopesha fedha kwa ajili ya mavuno na kurejesha baada ya mauzo.



Ukurasa 12

**Simulizi ya mama aliyeuweza uongozi mtaani kwake, ukahalalisha mapinduzi uchumi kwao**




Ukurasa 13

Safari ya Korea na mauzauza yake -I



Ukurasa 14

**Ushirika Nyanza una vyojipanga kuteka soko la pamba, kurejesha enzi zake**


# BUFE

IJUMAA JUNI 21, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


AKITANGAZA BAJETI YA NNE WIKI JANA...

# Sura kuu nne za Samia kutekeleza maendeleo



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akipokea Ripoti ya Kamati Maalum ya Corona, aliyoiunda, mwaka 2021. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Peter Orwa**

HADI sasa Serikali ya Awamu ya Sita ina hesabu ya miaka mitatu na ushee. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wiki iliyopita ikiwa mara ya nne ilisomwa bajeti ya serikali chini ya uongozi wake.

Wengi wamekuwa wakimfuatilia mwenendo wa zama zake za kiutendaji wana sura tofauti. Lakini katika mantiki ya saikolojia ya mwenendo wa uendeshaji uchumi wa nchi katika Awamu ya Sita ya Uongozi wa Maendeleo nchini, inaweza kugawanyika katika makundi makuu manne.

Mosi, ambako ndiko kwenye mzizi wake ni ilani, pia sera za chama chake CCM, uongozi uliopo ukielekezwa kutekeleza ndani ya kipindi maalum, ikwamo misimu ya uongozi.

Pili, ndani yake ni dira za kihistoria katika mipango ya maendeleo nchini, ambayo kwa kina inazama katika ubunifu uliofanywa baada ya uhuru; Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Tanzania 1964-1969, ikiambatana na yaliyoamuliwa makuu kitaifa, kuambatana nayo kwa wastani wa miaka minne mfululizo, hata ikadumu baada ya hapo.

Imani na dira ya kimaendeleo ya kudumu, ndio inayowawezesha Watanzania kufanikiwa kisekta maeneo kama elimu, kilimo na afya, imekuwa itikadi ya kudumu na ina historia tangu mwaka 1964, kuwafanikisha na ndio maana hata sasa Rais Dk. Samia, naye anaendeleza kulingana na mahitaji ya kisasa.

Mathalan, kwa sasa kuna wigo wa elimu bure, maboresho katika sekta ya afya kama bima ya afya, kuwawezesha wazee na kinamama katika nafasi hiyo, huku kukiwapo mapinduzi ya viwango vya huduma, kuanzia mindombinu, vifaa na utaalamu.

Hicho ndicho kinaonekana katika uwekezaji mkubwa katika sekta ya kilimo, bajeti yake ikikuzwa maradufu, kuleta mapinduz ya soko na teknolijia, kama ilivyo katika elimu, kubeba mfano Awamu ya Kwanza bajeti kufika asilimia 25.

Eneo lingine analotafsiriwa Rais Dk. Samia, inafafanuliwa katika mipango ya uongozi wake, una sura ya kuendeleza mazuri ya kimaendeleo yaliyojitokeza zaidi katika mfumo huria wa uchumi, hasa yaliyojiri Awamu ya Pili na Tatu ya uongozi wa nchi, ikikumbukwa Rais Benjamin Mkapa, akitamka 'serikali itabaki mratibu mkuu wa shuguli na biashara kubakia katika sekta binafsi.'

Lakini, penye sura ya nne anaporejewa Rais Dk. Samia ni katika staili ya uongozi na mipango yake ya maendeleo, daima hajaachana kitaaluma na alichukulia darasani; Utawala wa Umma, Uchumi na Maendeleo ya Kiuchumi.

Lakini, kama ilivyo msimamo wa viongozi wote wakuu wa nchi katika Awamu Tano zilizotangulia katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano, daima hazijawahi kuwa mbali na mtazamo mkuu wa misingi iliyoundwa na serikali ya Awamu ya Kwanza.

Hiyo imebaki kuwa dodosi kuu la sasa na awamu zote zilizotangulia, zimekuwa katika sura ya pamoja kutekeleza msingi wa Awamu ya Kwanza, kupitia Mpango wa Maendeleo wa Kwanza wa Mwaka 1964 na yaliyojitokeza baada ya hapo, mathalani miradi mikubwa ya kitaifa, reli ya SGR ambayo ina mzizi kuanzia zama za Awamu ya Tatu, pia mradi mkubwa umeme kutoka Awamu ya Kwanza

- ***Kuanzia Ijumaa wiki ijayo, fuatilia safari ya maendeleo tangu uhuru wa nchi, mageuzi ya mwaka 1964 na baada ya hapo.***

UCHUMI

DARASA LA USHINDI JINSIA KWA VITENDO…

# Simulizi ya mama aliyeuweza uongozi mtaani kwake, ukahalalisha mapinduzi uchumi kwao

• Apokea makofi ya wakazi, serikalini, siasa, wasomi na NGO

**Na Dk. Ananilea Nkya**

MWENYEKITI wa kijiji ni kiongozi muhimu sana katika nchi kwa sababu kiutawala anaingia kama mjumbe kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata (Ward Development Committee -WDC), ngazi ambayo ndipo vipaumbele vya bajeti ya halmashauri ya wilaya na vya taifa vinaanzia kupangwa.

Lakini kwa sasa, idadi ya wanawake wenyeviti wa vijiji ni ndogo sana na hivyo kuashiria kwamba nchi yetu inaendelea kuwa maskini hasa vijijini kutokana kukosekana kwa juhudi za kuhakikisha wanawake wenye sifa za kutoa uongozi bora vijijini wanapata fursa hizo sawa na wanaume.

Kwa mfano, wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani yenye kata 25 na vijiji na 125 ni kijiji kimoja tu cha Mwanambaya kilichoko katika Kata ya Mipeko ndicho ambacho mwenyekiti wake ni mwanamke ambaye anaitwa Leila Chamlumo.

Lakini huyu mwanamke mwenyekiti wa kijiji cha Mwanambaya amekuwa kiongozi wa kupigiwa mfano kwa utumishi uliotukuka kwa wananchi wa kijiji hicho na wilaya kwa ujumla.

"Chamlumo ametoa uongozi ambao umeleta maendeleo ya wananchi katika nyanja mbali mbali kwenye kijiji chake maana anajituma sana ni mwadilifu", anasema Prisca Ngwechemi, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Himiza Developemnt Organisation ambalo limefanya kazi za maendeleo ya wananchi wilayani Mkuranga kwa miaka mitano sasa.

Katika mazungumzo na mwandishi wa makala hii, Chamlumo anataja baadhi ya mambo makubwa ya maendeleo ya wananchi ambayo ameyasimamia yakatekelezwa kwa ukamilifu na ufanisi kuwa ni nafasi yake kama mjumbe wa WDC ni kusimamia mapato na matumizi ya halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, kuhakikisha kwamba fedha za kodi ya wananchi zinatumika kikamilifu kuleta maendeleo ya wananchi.

Anatoa mfano, alipoingia kwenye uongozi katika kijiji chake Mwanambaya zahanati ya kijiji hicho ilikuwa imechakaa kiasi kwamba paa lilikuwa linavuja akinena:"Mvua ikinyesha, daktari alilazimika kuondoka kwenye kiti chake na kwenda kujibanza eneo lingine."

Chamlumo anasema, aliamua kusimamia kikamilifu na kwa uaminifu mapato ya kijiji chake na kwa muda mfupi, kijiji kikafanikiwa kukusanya fedha shilingi milioni tano kwa ajili ya kukarabati zahanati hiyo.



Sehemu ya wakulima wilayani Mkulanga wakishughulika kuhudumia mashamba yao. **PICHA: MTANDAO**



Mwekikiti wa kijiji cha Mwanambaya, Leila Chamlumo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

> **"Vilevile tayari tumeshajenga jengo la makazi ya daktari na manesi na wanakaa hapa hapa kijijini kwetu kuwahudumia wagonjwa mchana na usiku.**

Pia, anasimulia kwamba alizungumza kampuni ya madini ya Songas, iliyochangia shilingi milioni 20 na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) ikatoa shilingi milioni tatu kabla ya yeye mwenyewe kupeleka ajenda hiyo kwenye kikao cha WDC, ambacho Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga nayo ilitoa bajeti ya shilingi milioni tano, jumla ya fedha hizo zikatumika kukarabati zahanati na kujenga wodi ya wajawazito.

"Nilipoanza kazi, zahanati ya kijiji chetu chenye vitongoji saba ilikuwa na kitanda kimoja tu kwa ajili ya wajawazito, lakini leo tuna wodi ya wajawazito na vitanda vya kutosha," anasema Chamlumo na kuongeza:

"Vilevile tayari tumeshajenga jengo la makazi ya daktari na manesi na wanakaa hapa hapa kijijini kwetu kuwahudumia wagonjwa mchana na usiku".

Kuhusu elimu, uongozi wa Chamlumo umeweza kukusanya fedha kutoka mapato ya kijiji na kwa sasa tofauti na miaka ya nyuma, kijiji cha Mwanambaya kilikuwa na shule moja tu ya Msingi Mwanambaya.

Anasema, kwa sasa wamejenga kwa fedha zao wenyewe zinazotokana na mapato ya kijiji shule mbili zaidi za msingi ambazo zitaanza kuchukua wanafunzi wakati wowote kuanzia sasa na tayari wamekwishanunua madawati 200 kwa ajili ya shule hizo zilizojengwa katika vitongoji vya Mizugu na Mivule

"Hizi shule zitawapunguzia wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda shule na kurudi nyumbani kwao," anasema Chamlumo na kwamba kijiji cha Mwanambaya kina vitongoji saba ambavyo ni Kiloweko, Madodo, Mizungu, Mamangwa, Kibeneke, Mabatini na Mivule.

Aidha, Chamluno anasema kazi kubwa nyingine ambayo amehakikisha mapato ya fedha za kijiji kutokana na vyanzo mbali mbali zimewezesha ni pamoja na kujenga ofisi kila kitongoji katika vitongozi vyote saba ili viongozi wa vitongoji hivyo waweze kufuatilia kwa karibu na kutatua matatizo ya wananchi na kuweka kumbukumbu za utendaji wao.

Anarejea alipochaguliwa mwenyekiti kwa mara ya kwanza mwaka 2006 akaunti ya kijiji ilikuwa na shilingi elfu 20 tu, lakini leo akaunti ya kijiji chake ina mamilioni kadhaa ya fedha.

"Kwa kweli ninamshukuru Mungu maana ninaamini ni kwa sababu utendaji wangu ndiyo sababu wananchi wa kijiji chetu wameendelea kunichagua tangu mwaka kwa miaka 15 sasa.

"Ila ninataka niwaombe kuanzia sasa nisogee mbele kwenye uongozi wa juu zaidi kwenye Kata nishughulikie Kata nzima ipige hatua ya maendeleo kama hiki kijiji chetu," anasema Chamlumo.

### NCHI ILIKO NA INAKOENDA

Hadi sasa, Chamlumo ni mmoja wa wanawake ambao wametoa mfano wa uongozi bora katika ngazi ya kijiji, takwimu zinaonyesha idadi ya wanawake wenyeviti wa kijiji ni ndogo mno hapa nchini na kama juhudi hazitafanywa na wadau mbalimbali.

Mfano unatolewa, serikali, vyama vya siasa, mashirika ya kiraia (NGOs) yanayotetea haki za wanawake, vyombo vya habari na wanahabari na taasisi za dini huenda uchaguzi ujao idadi ya wanawake wenyeviti wa serikali za vijiji iko ndogo inapaswa kuongezeka.

Swali kuu la kujiuliza ni: Je uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu 2024 utaongeza idadi ya wanawake wenyeviti wa vijiji hasa kwa kuzingatia kwa viongozi hao ni rasilimali muhimu sana kwa maendeleo ya vijiji?

Takwimu zinaonyesha kwamba, katika ngazi ya kitongozi ambayo ndiyo ya chini kabisa katika utawala wa nchi yetu idadi ya wanawake katika ngazi hiyo ni mdogo sana.

Nchini sasa kuna jumla ya vitongoji 62,612, ambavyo kwa mujibu wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwaka 2019 ni wanawake 4,171 tu walishinda nafasi za uenyekiti wa vitongoji sawa na asilimia 6.7.

Kwa upande wa mijini, ingetarajiwa kwamba wananchi wanaweza kuwa na uelewa mkubwa zaidi wa masuala ya demokrasia na hivyo idadi ya wanawake wenyeviti wa Serikali za mitaa, vijiji na vitongoji uwe ni mkubwa, lakini hali halisi ya ushiriki wa wanawake kwenye uongozi wa utawala wa Mitaa mijini bado ni duni sana.

Takwimu zinaonyesha kwamba wakati uchaguzi wa Serikali za Mitaa, vijiji na vitongoji ulipofanyika mwaka 2019 nchi ilikuwa na mitaa 4,171 ambapo wanawake waliochaguliwa kuwa wenyeviti wa mitaa ni 528 tu nchi nzima sawa na asilimia 12.6%.

Hali ya uongozi wa wanawake bado hairidhishi vijijini. Nchi nzima ina vijiji 11,915 ambapo wenyeviti wa vijiji wanawake ni 246 tu sawa na asilimia mbili nukta moja (2.1%).

Tafsiri ya idadi hii ndogo sana ya wanawake wenyeviti wa vitongozi, mitaa na vijiji ni kwamba maendeleo kijamii, kisiasa na kiuchumi katika ngazi za chini wanakoishi wananchi wengi bado ni changamoto kubwa sana hapa nchini na ndiyo sababu mamilioni ya wananchi wa taifa hili ni mafukara na wanaishi maisha yasiyo na furaha.

Taarifa ya dunia kuhusu hali ya furaha kwa wananchi, Tanzania mwaka huu 2024 imeshika namba ya 131 wakati mwaka jana 2023 ilikuwa nchi ya 129. Hii inaashiria kwamba hali ya wananchi wa Tanzania kutokuwa na furaha mwaka 2024 imepungua ikilinganishwa na mwaka 2023

### CHANZO CHA IDADI NDOGO

Mtaalam wa siasa na uongozi Dk. Victoria Lihiru, anataja tatizo mojawapo ni mfumo wa uchaguzi ambao umewapangia wanawake viti maalum, hivyo wanawake wenyewe na wanaume wa vyama vyote wamekuwa wakidhani nafasi za wanawake ni kwenye viti maalumu ni hali viti maalum lilikuwa ni suala la mpito.

Jambo lingine linatajwa kutokuwapo kwa Tume Huru ya Uchaguzi, inayomuwezesha kila mtu mwenye sifa za uongozi, bila ya kujali ni mwanaume au ni mwanamke au chama chake kuweza kugombea nafasi ya uongozi na kushinda au kushindwa kwa haki.

"Waziri wa TAMISEMI ambaye ni mwanasiasa na mwenye upande wa chama ndiye mwenye kauli ya mwisho kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, huyu hataweza kutenda haki kwa mgombea ambaye si wa chama chake", anasema William Maduhu, Ofisa Uchechemuzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

Vilevile vyombo vya habari, madhehebu ya dini na mashirika ya kijamii (NGOs), nazo zinatajkwa ni taasisi zisizofanyajuhudi kubwa kuelimisha na kuhamasisha jamii na wanawake wenye uwezo wa uongozi wajiunge kwenye vyama vya siasa na wagombee nafasi za uongozi katika Serikali za mitaa, vijiji na vitongoji ili kuweza kutoa uongozi wa kubadilisha maisha duni ya wananchi.

Katika nini kifanyike, watalamu wanashauri serikali ihakikishe inapeleka bungeni haraka Muswada wa Sheria itakayiowezesha uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji kusimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi ili wagombea wa vyama vyote, wanawake na wanaume watendewe haki maana kifungu cha 10 (1 c) cha Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi iliyopitishwa mwnzoni mwa mwaka huu ndivyo inavyoelekeza.


Lingine linatajwa ni Wizara ya TAMISEMI itoe mapema iwezekanavyo Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji kwa mwaka uliopo, 2024 na kuhakikisha kanuni hizo vipengene vyake vinatangwazwa kwenye vyombo vingi vya habari ili wananchi wafahamu kanuni hizo na wagombea waweze kujiandaa kikamilifu.

Vyama vyote vya siasa viandae idadi sawia ya wanawake na wanaume wenye sifa na uwezo wa kuwa viongozi bora wa vijiji, mitaa na vitongoji na kuhakikisha wanawake hao wanagombea nafasi hizo.

Mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za dini na vyama vya siasa watumie mikutano na vyombo vya habari kuhamasisha wanawake na wanaume wa rika mbali mbali waadilifu na wenye sifa za uongozi wajitokeze kugombea nafasi za uongozi wa vitongoji, mitaa na vijiji na kuwaelimisha kuhusu kanuni za uchaguzi huo kwa mwaka huu ili uchaguzi huo uipatie nchi yetu viongozi bora wanaume na wanawake katika nafasi hizo. Mungu ibariki Tanzania

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Safari ya Korea na mauzauza yake -I




NI takriban saa 12 jioni ya Mei 31 mwaka huu, tunatua kwenye uwanja wa ndege wa kijeshi wa Korea Kusini jijini Seoul. Hizo ni saa sita mchana za Bongo. Hapo ni baada ya kuruka jana yake kutoka uwanja namba moja wa Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Piga mahesabu tumekaa ndani ya lijidrimu hilo la Eitisi kwa muda gani. Mimi na baadhi ya walalahoi wenzangu ikiwa ni mara ya kwanza kupanda ndege tangu tuzaliwe.

Najikaza huku mwenzangu jirani naona kama anamwomba Muumba wake asijeumaliza mwendo ghafla.

Kabla hatujaruka Bongo, rubani anatwambia tutaruka juu kama meta 40,000 na ushei na umbali kutoka Dar mpaka Seoul ni zaidi ya kilometa 12,000.

Wakati tunatafakari na dege limesharuka umbali fulani hivi, mara kulakula inaanza! We acha tu ushamba mzigo! Nikitarajia jisahani la chipsi yai, kumbe...!

Tumeshiba, ghafla kila mmoja anakoroma akiwaza twendako ni wapi!

Najaribu kufikiria ndege aliyotumia Mfalme Zumaridi kwenda mbinguni kukutana na Mungu na kushuhudia vighorofa virefu vya dhahabu!

Naamini ilikuwa ni hii hii kwa uzuri wake! Kutoka mwendokasi mpaka ndege si mchezo eti!

Haya tukawa tumetua na kuchukuliwa hadi hotelini usiku.

Nashangaashangaa tu sijawahi kulala ghorofani. Nayaona maghorofa ya Seoul kama yale yale yaliyosimuliwa na Mfalme Zumaridi, marefuuu.

Nafikiria pengine nami huko ghorofani nitaonana na Mungu!Tunaambiwa kila mtu atalala chumba chake na anapaswa kukilipia! Wapi na wapi mgeni kulipia chumba cha kulala! Mimi naambiwa utalala chumba namba 902 huko juu, mwenzangu mwenye uzoefu na mambo haya ananiambia hapo ni ghorofa ya tisa na tunapanda kwa lifti!

Mambo ya lifti tena! Ikanikumbusha dogo aliyefyatuka siku moja hapa Bongo akikimbilia kupanda lifti, ilipofunguka akaingia haraka kumbe haikuwapo, akaporomoka na kuvunja mguu. Hofu ikanijaa ghafla, lakini nikajikaza.

Lakini tunaambiwa tena na wahusika; Wakorea wasiojua Kiswahili wala Kiingereza, wanatumia simu kujirekodi kwa Kikorea na simu inaandika Kiingereza, angalau tunaambulia mawasiliano.

Anasema leo mtalipa



**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

Won 90,000, wengine Won 110,000. Mimi nikaangukia kwenye won 110,000.

Ujue tu won moja ni sawa na takriban Sh. Mbili za madafu. Pia, tunaambiwa siku za wikiendi malipo yanabadilika kwani yanapanda na hakuna kulipa kwa dola ya Mmarekani, ambayo ndo tulikuwa nayo, lakini kama una kadi ya benki poa.

Wenye vyumba vya Won 90,000 watalipa Won 130,000, sisi wengine Won 180,000. Kichwa kikanizunguka, nikifikiria nitabaki na nini katika matumizi wakati najua hapa napita tu nitarejea Bongo.

Hapakuwa na jinsi, kila mtu akapanda lifti mpaka chumbani mwake, lakini udadisi ukatuonesha kuwa kumbe vyumba vya sakafuni hadi ghorofa ya pili havikuwa vinapangishwa wageni bali wenyeji waliokuwa wakifika jozi na kupumzika kwa muda na kuondoka, Bongo mnaitaje sijui!

Wenzetu hao walikuwa wakipewa vifaa mbalimbali kama miswaki, dawa, mafuta ya kupaka, vichokonoa masikio na 'zana', lakini sisi wengine tukiambiwa tujiju kama hujaja na mswaki wako itakula kwako, utatumia vidole.

Hakika siku ya kwanza yalinikuta hayo.

Asubuhi kuamka tunaambiwa hakuna stafutahi! Umewekewa birika, kahawa iliyochanganywa maziwa na sukari, maji, kahawa baridi ya kopo, chai baridi ya kopo na maji kwenye jokofu. Hivyo ni juu yako mwenyewe kujichemshia hakuna bufee!

Yaani nalipa maelfu na malaki hayo, lakini hakuna chai ya hoteli asubuhi, badala yake nafungua kinywa kwa kahawa na biskuti nne kweli?

Wanasema ndiyo maisha ya Wakorea hayo, walishajizoelea, ukitaka chai na supu unaingia mtaani. Labda, ndiyo sababu vitambi ni vya kusaka na darubini.

Ufanyeje mlalahoi, wewe unajichemshia maji unachanganya na kilichopo, unafungua kinywa kabla ya kufuatwa na dereva aliyetwambia anaitwa Paul (Mkorea anaitwa Paul sawa na Makonda! Mh kasoma Cuba) asubuhi kuingia mzigoni, mzigo uliotupeleka Korea, kumsaidia Mama katika masuala ya kufungua na kutangaza nchi.

Usiku unawadia tunarudishwa kunako hoteli yetu na kuona kama tutakula nini! Unaambiwa kula ni juhudi zako mtaani. Tulikofikia hapa ni Gasandong, wilaya ya Geumcheon, kila mtaa una mgahawa wa chakula. Chakula kikuu hapa ni nyama ya kuku, kitimoto, samaki na wali au mbatata.

Unachagua nini? Unafikiri nilichagua nini na walalahoi wenzangu? Wala sikutaka tena kula hotelini baada ya kutoka kwenye mgahawa huu tuliochagua siku ya kwanza kati ya tano tulizokaa Seoul. Bila shaka nitakwambia siku nyingine jinsi nilivyoipenda Korea Kusini na zaidi Seoul na hasa Gasan-Dong. We acha tu! Utanielewa tu wiki ijayo!

BIASHARA

# Ushirika Nyanza unavyojipanga kuteka soko la pamba,nia kurejesha enzi zake

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

SOKO huria, pia mtaji ni vikwazo na vigingi vinavyokitesa Chama Kikuu Cha Ushirika, Nyanza Cooperative Union 1984 Ltd (NCU), mkoani Mwanza, katika jitihada zake kuingia katika soko la ushindani dhidi ya kampuni binafsi zinazonunua zao la pamba.

Sasa, NCU imefikia uamuzi kuweka wazi mambo yake, ikisema sasa inajipanga upya kuhakikisha inaingia katika soko la ushindani mwakani, 2025.

Hapo inaweka mipango ya kuanzisha ndani yake, kampuni tanzu itakayokuwa ikinunua mazao mengine ya kibiashara .

Katika mazungumzo maalum na Nipashe, yaliyofanyika makao makuu ya chama hicho jijini Mwanza siku chache zilizopita, mara baada ya kuchaguliwa upya kukiongoza kwa miaka mitatu, Mwenyekiti mpya, Leonard Lyabalima ana ufafanuzi.

Anasema mateso hayo yameifanya NCU kushindwa kununua zao la pamba kwa msimu uliopo, kutokana na vigingi vinavyowakabili.




Wa tatu kutoka kushoto aliyeshika fimbo, ni Mwenyekiti wa Chama Cha Ushirika (Nyanza Co-operative Union 1984 (NCU) Leonard Lyabalima, akiwa na viongozi wapya wa chombo hicho, baada ya kuchaguliwa kukiongoza chama hicho kwa miaka mitatu, hivi karibuni. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

### CHANGAMOTO ZILIVYO

Lyabalima anasema changamoto kubwa inayoukabili ushirika huo, ni pamoja na ukosefu wa fedha za kuendeshea shughuli za ununuzi wa mazao ya kibiashara, hivyo yeye na viongozi wenzake wananuia kuweka utaratibu mzuri wa namna watapata mtaji kutoka taasisi za kifedha.

Vilevile wananuia kuhakikisha wanawaondolea mzigo mkubwa wakulima kuhangaika kutafuta masoko ya kuuza pamba, ikiwamo msimu uliopo zao hilo bei ya kilo moja imetangazwa kuwa shilingi 1060, ambayo haikidhi mahitaji yanayowasaidia kuwaondolea umaskini, hata wakajimudu kiuchumi.

Anakiri suala la bei ni mtambuka, likihusisha taasisi nyingi zinazopanga, hivyo cha msingi watatafakari namna ya kumsaidia mkulima itakapofika wakati sahihi kwa msimu ujao.

### MIKAKATI YAO

Lyabalima anasema,matarajio yake ni kwamba bodi iliyomchagua katika kuendesha gurudumu la ushirika, wananuia kuhakikisha chama NCU kinaimarishwa, wakibuni mbinu na mawazo mapya katika kununua pamba msimu ujao, yakiwamo mazao mchanganyiko kama vile dengu na mpunga.

Anaeleza mikakati yao mwaka uliopo, ni kufufua kiwanda cha kuchambua pamba Manawa kilichopo wilayani Kwimba, kuziba pengo la kutokuwapo viwanda vya pamba, huku akitaja mtaji na fedha taslimu ni miongoni mwa vigingi vinavyowakwamisha kufikia malengo hayo.

Vilevile, katika kuongeza thamani ya mazao wanayonuia kununua, wataegemea kutafuta fursa za masoko mengine nje ya nchi, kwa lengo la kumudu kuingia kwenye soko la ushindani, kukidhi shughuli za kibiashara zinazowaletea tija wanachama, pia wakulima wanufaika na ushirika tajwa.

"Tunajipanga upya, kwa sababu huwezi kuingia katika soko la ushindani wakati hakuna viwanda vya kuchakata pamba, hakuna mtaji," anaeleza Lyabalima, akiwa na ufafanuzi:

"Tunatarajia kufufua kiwanda kimoja cha Manawa kilichopo wilayani Kwimba, ili tuweze kuingia moja kwa moja kwenye ununuzi wa pamba na mazao mchanganyiko, tuweze kukabiliana na soko la ushindani."

Mtazamo wake ni kwamba, watajitahidi kadri ya uwezo wao, kuhakikisha kunakuwapo ufanisi wa mafanikio kukiinua NCU kiuchumi na kibiashara unakuwa wa hali ya juu, pia kuboresha bei zao hilo, ambayo bado iko chini kwa mkulima.

Anaeleza kuwa dunia ya sasa iko katika soko huria na ndiyo inayopanga bei, kinachotakiwa ni kujenga uwezo wa mtaji, ili kukabiliana na ushindani wa kibiashara, pasipo kuwapo changamoto yoyote.

### MJUMBE BODI

Gedion Majima, ni miongoni mwa viongozi wapya waliochaguliwa kuiendesha NCU ndani ya miaka mitatu, akiahidi kushirikiana na wajumbe wenzake kuinua ushirika huo, huku akigusia uhalisia kwamba,hali sio shwari ndani ya chama hicho kiuchumi.

Majima anaeleza kwamba, wao kukosa kununua zao hilo msimu uliopo, unakuwa pigo linalowasikitisha, ikiwamo wakulima, kwa sababu wanakiamini chama ushirika Nyanza kuuza mazao yao, akikiri kampuni binafsi za kununua pamba zimewafunika na kuwapiku kwa bei.

Analalamika NCU inakabiliwa na gharama kubwa za kuendesha shughuli za kununua pamba, huku bei ya bidhaa zake za ununuzi ziko, chini kuliko kampuni binafsi za ununuzi ambazo bei zake za kununua ziko juu.

Hivyo, anasema hilo linawafanya wajipange kupunguza gharama za uendeshaji, ili wawe na bei nzuri kwa mkulima hata kumkumbatia mkulima kuiuzia bei itakayomvutia aweze kwenda moja kwa moja kuiuzia NCU pamba zake.

Anasema, tangu kuingia soko huria mwaka 1994, kampuni binafsi ndio zikaanza kununua pamba kiholela, pasipo kujali usafi na ubora, hata thamani ya zao hilo katika soko la kimataifa ikaanza kushuka.

Majima anakumbusha historia, zamani kulikuwapo utaratibu wa ununuzi wa pamba kwa kufuata ubora; kulikuwapo viwango A na B, lakini viwango hivyo vimetoweka.

Anatia mtazamo kwamba, sasa lazima wahakikishe chama kinarudi katika hali yake ya kawaida kama zamani, wakikusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake vya kitega Uchumi, zikiwamo kodi za majengo na mali zingine, ili wajiendeshe kwa ufanisi, wamudu mikakati yao kiuchumi, badala ya kutegemea mikopo ya benki.

Pia, anasimulia NCU ilikotoka kihistoria, zamani Victoria Federation Union (VFU) iliyounda vyama mbalimbali vya ushirika katika mikoa baadaye mwaka 1973 vilivunjwa na kuwa Bodi ya Pamba, baadaye vikarudishwa na ikawa NCU.

Mpango wa kufufua viwanda nao sasa, unagonga kichwa chake, akiamini lazima ufanikiwe mwaka huu, ili msimu ujao waweze kununua pamba na mazao mchanganyiko wakipenya katika soko shindani ndani na nje ya nchi.

Anahitimisha kuwa, vita ya ushindani ni kikwazo kinachotakiwa kuondolewa wakishirikiana na serikali ya mkoa, itakayowasaidia kufikia malengo yao kiuchumi na kibiashara.

# TIRA yashtukia madai ya uongo ya bima

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imesema bado inakabiliwa na vikwazo vya baadhi ya watu kughushi madai ya kugongwa na vyombo vya usafiri ili kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Pamoja na vikwazo hivyo, TIRA imefanikiwa kuongeza idadi ya watumiaji bima nchini hadi kufikia milioni 12 sawa na asilimia 100imeongezeka kutoka milioni sita waliokuwepo mwaka 2021.

Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa TIRA, Hadija Maulid aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma.

Maulid, alisema moja ya jukumu la mamlaka hiyo ni kutoa elimu kwa umma ya umuhimu wa kuwa na bima ya mali na afya.

Alisema pamoja na kuongezeka watuamiaji wa bima nchini, zipo kero ikiwemo hiyo ya watu kughushi madai ya malipo ili wajipatie fedha.

"Soko la bima kwa sasa linakua sana, watu wanaendelea kukata bima kwa ajili ya mali zao, lakini kwa afya zao hadi sasa tumesajili watoa huduma za bima nchini zaidi ya 1,000," alisema.

Maulid, alisema watu hao wamekuwa wakigushi nyaraka kwa kutengeneza madai ya uongo kuwa wamegongwa na vyombo vya usafiri ili walipe fidia.

Alisema hilo ni kosa kisheria na mtoa huduma hapaswi kulipa malipo kwa kuwa siyo ya kweli.

Alilitaja jukumu jingine la TIRA kuwa ni kusimamia haki za kila mtu ambaye amekata bima kupata huduma anazostahili kutoka kwa watoa huduma.

"Moja ya jukumu letu ni kuhahakikisha kila aliyekata bima anapata huduma stahiki na kama anayo madai ambayo ni ya kweli anapaswa kulipwa," alisisitiza.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa madai ambayo yamekuwa yakiwasilishwa na kulipwa ni asilimia 95. "Hii inaonyesha katika madai 100, madai 95 yanalipwa kwa wakati na hii asilimia tano inayobakia ni ya kughushi lakini pia mengine, hivyo lazima ufanyike uchunguzi,"alisema

Alisema suala la wananchi kuwa na bima ni jambo la msingi kwani ni kinga dhidi ya majanga.

"Tunashauri wananchi kuwa na bima kwani itawaletea furaha pale watakapopatwa na majanga kwa mfano nyumba yenye thamani ya Sh. milioni 100 unalipa kiasi cha Sh. 177,000 kwa mwaka pamoja na VATm (Ongezeko la Thamani), "alisema

Meneja Utekelezaji na kushughulikia malalamiko wa Mamlaka hiyo, Okoka Mgavilenzi, alisema moja ya changamoto kwa jamii ni elimu kuhusu umuhimu wa kuwa na bima.

Mgavilenzi, alisema maeneo mengi nchini yamekumbwa na majanga kutokana na mvua za Elnino,

Ambayo kama wananchi wangekuwa na bima wangelipwa fidia na kuiondolea mzigo serikali wa kuwahudumia.

Hata hivyo, alisema mamlaki hiyo kupitia Skimu ya Bima ya Kilimo inafanya jitihada za kuwafikia wananchi katika maeneo ya vijijini ili waweze kukata bima ya mazao yao.




Mkuu wa Gereza la Isanga, ACP Zefania Neligwa (wa tatu kushoto), akipokea msaada wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vyenye thamani ya sh. milioni 24 kutoka kwa Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Kati, Sonia Mkumbwa, kwaajili ya matumizi ya gereza hilo, mkoani Dodoma, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kortini kwa mauaji ya walinzi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida, limewafikisha mahakamani Chacha Sandu (24) na Michael Steven (48), wakazi wa Bugugu Relini Mkoa wa Mwanza kwa tuhuma za mauaji ya walinzi wawili na kupora mali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Amon Kakwale juzi aliwaambia waandishi wa habari kuwa watuhumiwa hao walimefikshwa mahakamani baada ya kukamatwa wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga Mei 26, mwaka huu na kusomewa mashtaka hayo.

Kamanda Kakwale, alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kuwaua walinzi hao kwa nyakati tofauti Aprili 19, mwaka huu katika Kata ya Misuna Manispaa ya Singida.

Alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kumuua Elvis Muna (65), baada ya kumvamia wakati akilinda duka na kuiba vitu mbalimbali, ikiwemo simu ndogo mbili aina Tecno, smartphone mbili Infinix na Sumsung.

Kakwale alisema watuhumiwa hao, pia wanadaiwa kumuua Ismail Ramadhan (37), mlinzi wa Kampuni ya New Imara baada ya kumvamia wakati akilinda grosari ijulikanayo kwa jina la 'Supa kitasa' kwa lengo la kuiba na kutokomea kusikojulikana.

# WOWAP lajitosa ukatili wanawake

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la WOWAP limezindua Mradi wa Mwanamke Salama kwa ajli ya kutoa elimu kwa jamii ili kupunguza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto nchini.

Mratibu wa WOWAP, Warda Shayo, alisema mradi huo unatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa ajili ya kuwanusuru wahanga wa ukatili wa kijinsia na kuwaweka salama.

Shayo, alisema wamewekа mikakati ya kuhakikisha wahanga hao, wanapata haki na kuepuka vitendo vya ukatili dhidi yao katika jamii.

"Ukatili unachangia kwa kiasi kikubwa kukatiza ndoto za watoto wa kike. Mradi huu utasaidia kutokomeza ukatili wa kijinsia mkoani hapa"alisema

Aliipongeza serikali kwa kutoa ushirikiano kupingaji ukatili na kuwarahishia kutekeleza majukumu yao.

Ofisa Ustawi wa Jamii na Mratibu wa One Stop Centre Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Dodoma, Elvira Mutagwaba, alitaja moja ya changamoto wanazokutana nazo ni kesi kutokamilika kwa kukosa ushahidi.

Mutagwaba, alisema kesi hizo zinakwamishwa na ushahidi kutoka kwa ndugu na waathirika wa vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia.

Aliiomba jamii kutoa ushirikiano kwa taasisi zinazopinga ukatili wa kijinsia ili watuhumiwa wakamatwe na kufikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Mutagwaba, aliiomba mahakama iangalie namna ya kutatua kesi za ukatili wa kijinsia.

Mwakilishi wa Dawati la Jinsia wa Jeshi la Polisi, Amina Mzee, aliwataka wazazi kuongea na watoto kuhusu ukatili wa kijinsia.

Mzee, alisema ukatili huo pamoja na kuanza kupungua, bado vitendo hivyo vinafanywa na watu wakiwemo ndugu wanaokaribishwa nyumbani.

Aliwataka wazazi kuacha tabia ya kuwalaza watoto wa kiume na kike chumba kimoja kwani ndiko ukatili unakoanzia kwa majumbani.





# H'shauri yapewa jukumu kutokomeza utoro shuleni

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

HALMASHAURI ya Mji wa Makambako mkoani Njombe imetakiwa kupambana, kutokomeza vitendo vya utoro kwa wanafunzi wa sekondari ambako kunasababisha wengi kuacha shule.

Katika halmashauri hiyo mwaka wa 2022 idadi ya wanafunzi wa sekondari walioacha shule ni 265.

Hayo yalibainika katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Makambako lililolenga kujadili hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ofisa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Mkoa wa Njombe, Willy Nodule alisema kuwa idadi ya watoto 265 kuacha shule ni wengi, hivyo kuitaka idara ya elimu kupita kila kaya kuelimisha ili wanafunzi warudi shule.

"Tunaomba tujitahidi kwa hilo Mh. Mwenyeki na Mkurugenzi ili kuhakikisha watoto hawa wanarudi shule, lakini kuna shule ambazo zimeanguka sana nimezianzisha hapa kuna shule za Sekondari Kipagamo, Lyamkena, Kitandililo, Mukilima, Mhongole na Makambako," alisema Nodule.

Mkaguzi huyo alisema idadi kubwa hiyo ya wanafunzi waliacha shule kabla hawajafika kidato cha nne.

Hata hivyo, aliwapongeza kwa kuwa na hati ya umiliki wa Shule ya Sekondari Kitandililo.

"Sio shule hii ya Kitandililo tu ilikuwa aina hati, kuna shule zipo katikakti ya mji unajua hapa mjini kuna mtu anazidi hatua moja mnakuja kushtuka shule imeshabanwa alafu mwenzio katangulia, tunaomba na hili mliangalie mkurugenzi," alisema Nodule.

Awali akizungumza wakati akiwasilisha taaria ya hoja ya CAG, Mtunza Hazina wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Hassan Kisenge alisema kuna hoja ya wanafunzi kuacha masomo kabla hawajamaliza shule.

Baada ya kikao hicho, Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Mji Makambako, Adel Kinombo alisema ujenzi wa shule za kata umepunguza utoro wa wanafunzi hivi sasa.

Alisema: "Changamoto ya kwanza wanafunzi walikuwa wanatembea umbali mrefu walikuwa wanatembea kilometa zaidi ya nane na kuna wanafunzi ambao walikuwa wanakaa mbali na shule lakini changamto hizo zimeendelea kutatuliwa baada ya kuanza ujenzi wa shule mpya".




Mkurugenzi wa Mawasiliano na Mifumo wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Japhet Boaz (kushoto), akizungumza na baadhi ya walengwa wa mfuko huo, wakati wa maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika viwanja ya Chinangali Park, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC: Ludewa ina madini, itakuza uchumi wa taifa

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka amesema Wilaya ya Ludewa inabahati kuwa na madini ya makaa ya mawe na chuma, jambo ambalo litakuza uchumi wa mkoa na taifa kwa ujumla.

Mtaka aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari wilayani hapa.

Alisema uwepo wa madini hayo unakwenda sambamba na kuanza kwa mradi wa liganga na mchuchuma.

"Ni kwamba maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan yatakapokuwa yametekelezwa mradi huu kama tunavyouona, siyo kwamba utabadilisha uchumi wa mkoa lakini pia utabadilisha uchumi wa nchi yetu kwa sababu mradi wa mchuchuma na liganga umetajwa pia kwenye Dira ya Taifa ya Mwaka 2025-2050," alisema Mtaka.

Alisema nchi nyingi duniani wanachimba chuma zaidi ya mita 15 kwenda ardhini, lakini bado Tanzania inaneema ya kuwa na milima inayobeba chuma upande mmoja na mlima mwingine unabeba makaa ya mawe.

Alisema kutekelezwa kwa mradi wa linganga na mchumama utaleta unafuu kwenye soko la chuma duniani.

"Matarajio yetu sisi watu wa Njombe kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan amezungumza wakati akiwa kwenye ziara mwaka 2022 matamanio yake ni kuona chuma haitoondolewa hapa kama chuma ghafi, chuma hii itapelekea kujengwa kwa viwanda vinavyoongeza thamani ya madini haya ya chuma," alisema Mtaka.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari alisema pindi mradi huo utakapoanza viwanda mbalimbali vitawekezwa nchini na ndiyo maana mazungumzo ni marefu kwa sababu unapaswa kuwanufaisha wananchi.

Katibu wa Siasa na Uenezi CCM Mkoa wa Njombe, Josaya Luoga alisema dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan inakwenda kutimia, kwamba mradi wa liganga na mchuchuma unakwenda kutekelezwa baada ya kulipa fidia wananchi.

# Mfumo wa kidijitali waleta mageuzi wanufaika TASAF

**Na Faustine Feliciane**

MABADILIKO ya mfumo wa utoaji huduma kwa walengwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuhamia kwenye teknolojia ya kidijitali imetajwa kuongeza ufanisi katika shughuli za mfuko huo.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa mfuko huo, Japhert Boaz, aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya wiki ya watumishi wa umma.

Alisema tangu mfuko huo kuhamia kwenye utoaji huduma kwa njia ya mtandao kuna ufanisi mkubwa na kuwafikia walengwa kwa wakati.

Boaz alisema kabla ya mfumo huo walengwa ambao ni kaya maskini ilikuwa inawachukua kati ya siku 20 mpaka 26 kupata huduma za malipo ya ruzuku baada ya kutumwa kwa halmashauri husika.

"Kwa sasa baada ya kufanya malipo inachukua saa 48 tu kwa walengwa wetu kupata ruzuku zao, kwa sasa tunatumia mifumo ya benki au simu za mkononi kutuma moja kwa moja fedha kwa wananchi walengwa, kabla ya hapo tulikuwa tunatuma kwa halmashauri, inachikua muda kufika na hata zikifika pia kulikuwa na muda mrefu mpaka walengwa kupata fedha zao, kiufupi mchakato wa awali ulikiwa mrefu zaidi," alisema Boaz.

Alisema wanahudumia zaidi ya kaya milioni moja nchi nzima na zipo kaya zilizonufaika na kufikia kujitegemea bila kuhitaji tena ruzuku za TASAF.

"Katika huduma zetu pia tunatoa mafunzo mbalimbali ya kijasiriamali, zipo kaya ambazo sasa zinajiendesha zenyewe kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali na kuziuza, wapo wenye mifugo, wapo ambao wanazalisha vitu kama sabuni na mafuta ya alizeti na kuyaendesha maisha yao," alisema Boaz.

Kuhusu maadhimisho ya wiki ya utumishi wa umma, alisema wanayatumia kuwajengea uwelewa wananchi juu ya shughuli wanazozifanya.

Alisema: "Hapa tunatoa elimu, tunapokea kero, maoni na ushauri, lakini kikubwa na kuwaelimisha wananchi juu ya huduma zetu, lakini pia huduma zote zinapatikana kwenye banda letu hapa kwenye maadhimisho".



## Maghala ya kuhifadhi chakula kujengwa kukabili njaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis amesema wizara yake inatarajia kujenga maghala mawili ya kuhifadhi chakula, ili kukabiliana na uhaba wa chakula unaoweza kusababisha maafa.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla Ameir aliyetaka kujua mikakati ya serikali katika kukabiliana na uhaba wa chakula kwa kujenga maghala ya kuhifadhi chakula.

Waziri huyo alisema uhifadhi wa chakula ni muhimu ili kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa chakula unaoweza kusababisha maafa ikiwemo kwa watoto.

Alisema maghala ya chakula yanatarajiwa kujengwa eneo la Chamanangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba pamoja na Binguni Wilaya ya Kati Unguja.

Alisema maghala hayo yatakuwa na uwezo wa kuhifadhi tani za chakula 60,000 ambapo kazi ya ukarabati imeanza pamoja na ukarabati wa maghala yalipo Malindi Unguja.

Aidha, aliwataka wakulima kuongeza juhudi za kulima chakula chenye kustahimili mazingira ya ukame ikiwemo mtama na mahindi.

Alisema kilimo cha mazao hayo hivi sasa kimezorota sana ambacho ni kizuri kutokana na kustahimili mazingira ya ukame ambacho hulimwa katika ardhi ya mawe.

Waziri Ameir alisema: "Katika kukaabiliana na uhaba wa chakula serikali ikijenga maghala zaidi ya kuhifadhi chakula tunawaomba wakulima wetu kuongeza uzalishaji ambao utatuwezesha kukabiliana na changamoto za uhaba wa chakula".

# Amani, usalama kujadiliwa mkutano wa IPU Geneva

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson amesema hoja kubwa ambayo itatawala katika mkutano wa wabunge wa umoja huo jijini Geneva Oktoba mwaka huu ni amani na usalama.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar baada ya kumaliza mkutano na viongozi wa IPU na kufanya ziara katika vivutio mbalimbali vya utalii visiwani hapa.

Alisema zipo nchi nyingi ambazo zinachangamoto ya vita, hivyo wataangazia maeneo yote yenye changamoto hiyo na kuisimamia serikali kuhakikisha wanaelekeza nguvu katika masuala ya ulinzi, usalama na amani.

Alisema pia watajadili akili mnemba pamoja na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri nchi nyingi duniani, hivyo lengo la kujadili mikakati hiyo ni dunia kuendelea kuwa salama na kuepukana na athari.

Dk. Tulia alisema katika mkutano huo wamepitisha sera ya udhalilishaji ili kila mtu kuwa salama pamoja na hoja ya akili mnemba.

Alisema kuna haja ya kufanya utafiti katika eneo hilo kwa sababu linaleta maendeleo upande mmoja lakini upande mwingine linaleta changamoto.

Akizungumzia kuhusu ziara waliyoifanya jana kutembelea vivutio vya utalii ikiwamo Mji Mkongwe wa Zanzibar, alisema viongozi hiyo wamejifunza vitu vingi ikiwemo historia ya Zanzibar ikiwemo biashara ya utumwa. Hivyo, aliwataka Watanzania kuendelea kuvitunza vivutio vya utalii na sehemu za historia ambazo zinaliweka taifa katika mazingira ya faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya ziara hiyo, viongozi hao walisema kuwa wamefurahishwa na mandhari ya Zanzibar pamoja na uwepo wa hali ya amani na usalama.

Viongozi hao walitembelea katika Mji Mkongwe na kujionea maeneo ya kihistoria yaliokuwa yakifanyika biashara ya utumwa ikiwemo katika Kanisa la Anglikana la minara miwili.



Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wanne kushoto), akiwa ameongozana na baadhi ya viongozi wa umoja huo, walipotembelea vivutio vya utalii katika Mji Mkongwe wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sekta ya utalii inachangia 30% pato la Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema sekta ya utalii ni muhimu kwa ustawi wa taifa, kwa sababu inachangia zaidi ya asilimia 30 ya pato la taifa la Zanzibar.

Aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa programu ya hakuna matata ambayo inalenga kuboresha uzoefu wa watalii wa kigeni wanaotembelea visiwa vya Unguja na Pemba.

Waziri Soraga alisema utalii ni sekta mama na inachangia asilimia 80 ya fedha za kigeni na inatoa ajira zaidi ya asilimia 60 ya ajira zote katika mnyororo wa thamani.

Alisema lazima sekta hiyo kupewa kipaumbele kwa kuwa ni sekta ambayo inamageuzi makubwa, hivyo ni vizuri kuendana na wakati wa mageuzi hayo.

Alisema huduma hiyo itaongeza thamani ya sekta hiyo na kurahisisha wageni wanapofika kupata huduma za mawasiliano za uhakika na kufanya miamala.

"Huduma hii pia itatusaidia sisi wizara kutambua maeneo ambayo watalii wanatembelea, kama kuna eneo ambalo tunapata tabu sana katika utalii ni katika takwimu kujua wageni wangapi wameingia," alisema.

Hivyo, alizitaka sekta binafsi kushirikiana na serikali katika kuhakikisha kupata takwimu zinazoonesha uhalisia tangu mgeni anapokuja, sehemu anazoenda kuzitembelea ambapo itasaidia kuboresha sekta hiyo.

Aidha alisema kampuni ya Tigo Zantel, inamchango mkubwa wa kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya mawasiliano kwa muda mfupi katika kuboresha dhana ya mawasiliano katika visiwa vya Zanzibar. Alisema serikali ipo katika hatua za mwisho za kutoa huduma za viza kwa njia ya kidijitali ili kwenda na wakati wa ukuaji wa Tehama ambayo itashajihisha kupata huduma viza kwa haraka na kupata watalii wengi zaidi kufika Zanzibar.

Ofisa Mkuu wa Biashara wa kampuni ya Tigo Zantel, Isaack Nchunda, alisema dhamira ya kampeni hiyo ni kuchangia kwenye ajenda ya Serikali ya Zanzibar ya kuhakikisha kuwa watalii wanapofurahia vivutio vilivyoko visiwani hapa wanaendelea kuwasiliana na kushea vivutio hivyo na ndugu, jamaa na dunia kwa ujumla kupitia vifurushi vipya vya jambo pack.

"Vile vile, kupitia kampeni ya hakuna matata, tutaingia ubia na hoteli, mamlaka za viwanja vya ndege pamoja na migahawa maarufu hapa Zanzibar ili kuhakikisha kuwa huduma na bidhaa zetu zinawafikia watalii wetu katika maeneo watakayokuwepo hapa visiwani kwa haraka na usalama zaidi" alisema.

Aidha alisema wageni wanahitaji kuwasiliana na familia zao, marafiki na kuonyesha uzuri na maajabu ya Zanzibar kwa dunia nzima na ndio sababu wamejidhatiti kuhakikisha kuwa wageni wanapata huduma bora na za kipekee ambazo zitawawezesha kuwasiliana kwa urahisi zaidi.

# Ziara ya Putin Asia Mashariki yaongeza hofu kwa Marekani

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, ameanza ziara ya kiserikali nchini Vietnam, baada ya kumaliza kuitembelea Korea Kaskazini.

Kiongozi huyo anafanya ziara katika mataifa kadhaa ya Asia Mashariki.

Akiwa nchini Vietnam, amekutana na kufanya mazungumzo na mwenyeji wake Rais To Lam na viongozi wengine wa chama cha kikomunisti.

Hata hivyo, Marekani imekosoa ziara ya Rais Putin katika nchi ya Korea Kaskazini na mataifa mengine ya Asia, ikisema inataka kuzifanya nchi hizo kama jukwaa la uungwaji mkono wa Russia katika vita vya Ukraine.

Nchi ya Vietnam bado inathamini uhusiano wake wa kihistoria na Russia, licha ya jitihada zake za kuboresha ushirikiano na mataifa ya Ulaya na Marekani.

Uhusiano wa Vietnam na Russia ulianza miongo mingi iliyopita, ikipewa misaada ya muhimu ya kijeshi, kiuchumi na kidiplomasia. Kipindi hicho ilijulikana kama jimbo jipya la kikomunisti Vietnam Kaskazini katika miaka ya 1950.

Rais Putin alimaliza ziara yake nchini Korea Kaskazini jumatano na kupata nafasi ya kukutana na kiongozi wa taifa hilo Kim Jong Un na kutiliana saini ya makubaliano ya kulindana iwapo nchi zao zitakabiliwa na vitisho kutoka nje.

Wakati huo huo, Japan imesema ina wasiwasi kuhusu makubaliano yaliyofikiwa kati ya Korea Kaskazini na Russia.

Msemaji wa serikali, Yoshimasa Hayashi, alisema makubaliano hayo ambayo hutoa msaada wa pande zote katika tukio la uchokozi kwa nchi moja ni kitendo kinachoteleta hofu.

„Japan ina wasiwasi kutokana na ukweli kuwa Rais Putin hajaondoa ushirikiano wa kijeshi na kiufundi na Korea Kaskazini," alisema Hayashi wakati wa mkutano na waandishi wa habari.

Alisema ushirikiano wa aina hiyo unaweza kujumuisha ukiukaji wa moja kwa moja wa maazimio husika ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, katika suala la athari zake kwa mazingira ya usalama ya nchi ya Japan na kanda.

Jumatano ya wiki hii, Rais Putin alielezea makubaliano kati ya nchi hizo mbili zilizoungana sawa na hati ya mapinduzi ya kweli, hivyo Russia haijaitenga Korea Kaskazini kijeshi na kiufundi.

***BBC***



Maofisa wa usalama wakimsaidia mtu aliyepoteza fahamu baada ya kuzidiwa na joto kali wakati wa ibada ya Hija nchini Saudia Arabia. **PICHA: AP**

# Joto laua mahujaji 900

**MAKA,** SAUDIA ARABIA

JUMLA ya mahujaji 900 walifariki wakati wa Hija, idadi kubwa kutokana na wimbi la joto kali lililofikia nyuzi 51.8.

Kulingana na mwanadiplomasia mmoja kutoka nchi za Kiarabu, wengi waliopoteza maisha ni raia wa Misri waliofikia 800.

Hata hivyo, baadhi ya nchi zimethibitisha kuwa miongoni mwa mahujaji waliokufa ni kutoka kwenye mataifa hayo. Nchi hizo ni Jordan, India, Indonesia, Iran, Senegal, Tunisia na Kurdistan ya Iraq.

Imeripotiwa kuwa ndugu na jamaa za mahujaji waliotoweka wakati wa ibada ya hija nchini Saudia Arabia walikuwa wakiwatafuta wapendwa wao katika hospitali wakihofia kuathirika na hali mbaya ya hewa.

Ilielezwa Idadi kubwa ya mahujaji waliofariki wakati wa ibada ya Hija wiki iliyopita katika mji wa Mecca,ambao ni mtakatifu zaidi kwa waumini wa Kiislamu ni raia wa Misri.Hapo awali, wanadiplomasia wengine waliripoti kuwa raia wa Misri 323 walifariki wakati wa ibada hiyo, ambayo ilihudhuriwa na karibu watu milioni 1.8 mwaka huu, wengi wao kutoka nje ya nchi.

***RFI***

# Israel yashambulia kambi ya wakimbizi

**GAZA,** PALESTINA

VIKOSI vya jeshi la Israel vimeendelea kushambulia maeneo ya katikati mwa Ukanda wa Gaza na kusababisha vifo vya watu watatu.

Taarifa kutoka Gaza zilieleza, watu wengine kadhaa wamejeruhiwa katika mashambulio yaliyofanyika usiku wa kuamkia juzi.

Ndege za kijeshi pia ziliishambulia kambi ya AL-Nuseirat na kumuua mtu mmoja na wengine 12 waliachwa wakiwa majeruhi.

Taarifa hiyo ambayo ilitolewa na wahudumu wa hospitali ya Gaza, ilieleza vifaru vya Israel pia vilishambuliwa kwa mizinga kwenye kambi za Al-Maghazi na Al-Bureji.

Kambi hizo ni za kihistoria katika eneo la Ukanda wa Gaza.

Jeshi la Israel limesema vikosi vyake vinaendelea na operesheni katika eneo hilo likiwalenga wanamgambo wa Hamas na kuiharibu miundombinu yao ya kijeshi katika hatua ambayo ilisisitiza ni sahihi, na inafanyika kutokana na taarifa za intelijensia.

***DW.***

**Taarifa hiyo ambayo ilitolewa na wahudumu wa hospitali ya Gaza, ilieleza vifaru vya Israel pia vilishambuliwa kwa mizinga kwenye kambi za Al-Maghazi na Al-Bureji.**

# Maandamano yatikisa Kenya kupinga ongezeko la kodi

**NAIROBI,** KENYA

RAIA wa Kenya wamefanya maandamano jana kupinga mapendekezo ya ongezeko la kodi katika muswada wa sheria ya fedha ambao wengi wanahofia litazidisha gharama za maisha.

Serikali ya Rais William Ruto, ambayo inakabiliwa na uhaba wa fedha, ilikubali kufanya mabadiliko ya sheria hiyo baada ya mamia ya waandamanaji kupambana na polisi jiji la Nairobi, kuanzia juzi.

Hata hivyo, serikali bado iliendelea na hatua za kuongeza kodi na kutetea nyongeza zilizopendekezwa ikisema zinahitajika ili kupata fedha kwa ajili ya kupunguza utegemezi wa kukopa kutoka nje.

Hata hivyo, waandamanaji waliapa kuendelea kuingia barabarani katika mikoa yote nchini humo kuzuia ongezeko hilo la kodi. Bunge la Kenya lilitarajiwa kupigia kura muswada huo mpya jana, licha ya raia wengi wao wakiwa vijana wakiandamana kuupinga.

Maandamano hayo ambayo yalianza Jumanne wiki hii yamesababisha kukamatwa kwa watu kadhaa katika jiji la Nairobi.

Licha ya Nairobi, maandamano haya yamefanyika katika miji mingine mbali mbali ya nchi hiyo.

Wanasheria na makundi ya haki za binadamu walishutumu polisi kwa kutumia nguvu kubwa dhidi ya watu wanaoandamana kwa amani.

Awali Rais William Ruto, alisema serikali yake inahitaji fedha zaidi ambazo zitatokana na ukusanyaji kupitia kodi ili kupunguza deni la taifa ambalo ni zaidi ya dola bilioni 70.

***BBC***

# EDNA LEMA ATAJA SABABU KUONDOKA BIASHARA UNITED

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA Edna Lema juzi jioni alitangaza rasmi kuachana na klabu ya Biashara United huku akisema sababu kuondoka ni kumalizika mkataba wake na kuhitaji changamoto mpya.

Edna alikuwa kwenye benchi la ufundi la klabu hiyo iliyoshiriki Ligi ya ‚Championship' kama kocha msaidizi.

Akizungumza juzi akiwa njiani kutoka Mara, Edna alisema hakuna mtu anayeacha kazi na kuaga huku asijue wapi anakwenda hivyo watu watajua tu wapi nitaenda.

„Kazi Biashara imeisha, nimemaliza mkataba na sasa narejea Dar es salaam kwa ajili ya mambo mengine, kama kuna timu naenda basi itajulikana tu muda sahihi ukifika," alisema Kocha huyo wa zamani wa timu ya wanawake ya Yanga, Yanga Princes.

Edna aliishukuru klabu hiyo ya Mkoani Mara kwa kumuamini na kumpa nafasi ya kuwa sehemu ya benchi lao la ufundi.

Edna aliisaidia timu hiyo kucheza hatua ya ‚play off' kuwania kufuzu kucheza Ligi Kuu Tanzania bara lakini haikufanikiwa baada ya kufungwa na Tabora United.

Hata hivyo kocha huyo kwa siku za karibuni amehusishwa tena kutaka kurejea kwenye klabu ya Yanga Princes baada ya kufikia makubaliano na uongozi wa klabu hiyo.

**Wasanii wa kikundi cha Mwalimu Steph Sanaa Group, wakitoa burudani wakati wa kuzindua mradi wa ‚Tayari kwa ajira jumuishi endelevu na ujasiriamali', unaofadhiliwa na Standard Chartered iliyofanyika, jijini Dar es Salaam jana. PICHA: JUMANNE JUMA**




# NYOTA WA ZAMANI YANGA WAWANOA VIJANA

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI wa zamani wa klabu ya Yanga juzi waliungana na vijana wanaounda kikosi cha timu ya ‚Safari Champion Cup' na kuwapa mbinu mbalimbali kuelekea kwenye mchezo wao maalum dhidi ya kikosi cha mabingwa hao wa soka Tanzania Bara.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jioni Avic Town, Kigamboni ambapo ndipo mahali timu hiyo ilipo weka kambi yake, Ofisa Habari na Mawasiano wa Klabu ya Yanga, Ally Kamwe alisema lengo la wachezaji hao kwenda kambini hapo ni kuwapa mafunzo na mbinu ya kimichezo ili miaka ijayo wapatikane wachezaji wazuri wa Taifa.

„Hawa wachezaji wa zamani watawapa mbinu na mafunzo ambayo naamini yatawasaidia kufanya vema kwenye mchezo huo ambao utakuwa na burudani ya aina yake, alisema Kamwe.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Mashindano wa Yanga, Sadi Kawemba aliwataka vijana hao kuhakikisha wanapambana ili watimize malengo yao.

"Pambaneni mhakikishe mnatimiza malengo yenu kwa kufanya vizuri katika mchezo huo na kufuata yale mtakayofundishwa na wachezaji wa zamani na makocha wenu, michezo hujenga afya vile vile itawasaidia kupata ajira," alisema Kawemba.

Wakati huo huo Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kupitia kwa Ofisa habari wake, Cliford Mario Ndimbo imeipongeza Kampuni ya Bia Tanzania( TBL) kwa kutafuta vijana wenye vipaji kutoka mikoa mbali mbali na kufanikiwa kupata idadi ya wachezaji 22.

Aidha alisema TFF wapo tayari kushirikiana na taasisi yoyote yenye nia ya kuendeleza soka la vijana hapa nchini kwa kuwa wanatambua michezo ina thamani kubwa.

Vile vile aliwapongeza wachezaji wote waliopata fursa ya kuitwa katika timu hiyo baada ya kufanyiwa mchujo na viongozi wao.

Kikosi hicho cha viajana kinatarajia kucheza mchezo maalum wa kirafiki dhidi ya Yanga Juni 29 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

## Kuogelea waenda Kenya mashindano ya Kimataifa

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha waogeleaji wanne wa timu ya Taifa ya mchezo huo kinatarajiwa kuondoka leo kuelekea Nairobi, Kenya kwa ajili ya kushiriki mashindano ya kimataifa yatakayoanza Juni 23 kesho nchini humo.

Akizungumza na waogeleaji hao jana wakati akiwakabidhi bendera ya Taifa, Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Abel Odena aliwataka wanamichezo hao kwenda kupambana kuhakikisha wanarudi na medali za ushindi nyumbani.

„Nendeni mkapambane kuhakikisha mnakwenda kuipeperusha vema bendera ya Taifa kwa kupata medali nyingi za dhahabu kwani kila kitu kinawezekana," alisema Odena.

Kwa upande wake Kocha Mkuu wa timu hiyo, Alexander Mwaipasi alisema watakwenda kushindana kwa kutumia bwawa la mita 50.

„Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunakwenda kufanya vizuri katika mashindano hayo ambayo naamini yatakuwa na ushindani kwa kuwa wachezaji wetu wamezoea kuogelea kwenye bwawa la mita ishirini na tano," alisema Mwaipasi.

Aidha aliwataka watanzania waendelee kuwaombea ili waweze kwenda kutimiza malengo yao katika michuano hiyo itakayoshirikisha nchi mbalimbali.

## CAG, SHYCOM waandaa mbio za hisani

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAHITIMU wa Chuo cha Ualimu Shinyanga (SHYCOM) akiwamo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, wanatarajia kufanya mbio za hisani Septemba 21 mwaka huu kwa lengo la kuchangisha fedha za kukarabati miundombinu ya chuo hicho.

Akizungumza kwa niaba ya wahitimu wa chuo hicho, CAG Kichere alisema wamekuja na tukio hilo ili kuunga mkono juhudi za Serikali za kuboresha miundombinu ya elimu na kurejesha kwa jamii kile wanachokipata.

„Tunaomba watanzania watuunge mkono kwenye tukio hili, natoa wito kwa wanafunzi wengine wote waliopita chuo cha SHYCOM tuungane kwa pamoja tuiweke vizuri miundombinu yake,"alisema Kichere.

Naye, Mratibu wa kamati ya maandalizi ya mbio hizo, Arnold Bwechum, alisema lengo ni kufanya hamasa katika umoja na mshikamano miongoni mwa wanafunzi waliosoma chuo hicho.

Mkuu wa chuo hicho, Dk. John Nandi, aliwapongeza wanafunzi hao kwa uamuzi wa kufikiria kukarabati miundombinu ya chuo hicho ikiwamo njia za watu wenye ulemavu.

Mbio hizo zimepewa kauli mbiu ya 'Kata upepo kwa afya kuiboresha SHYCOM'.

==

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GREENWOOD AWANIWA LAZIO
LAZIO imeanza mazungumzo na Manchester United kuhusu uhamisho wa pauni milioni 30 kumnunua mshambuliaji wa zamani wa England, Mason Greenwood mwenye miaka 22. ***(Mail)***

### JUVE, NAPOLI NAZO WAJITOSA
JUVENTUS na Napoli pia zinawania kumsajilia Mason Greenwood. ***(Independent)***

### BRUNO KWENYE RADA
ARSENAL wanaweza kutafuta ofa ya kumtoa mchezaji pamoja na fedha ili kumnunua kiungo wa kati wa Newcastle na Brazil Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Transfers)***

### OLISE AWA LULU
LIVERPOOL inalenga kuzishinda Chelsea na Manchester United katika kumsajili winga Mfaransa Michael Olise mwenye miaka 22, kutoka Crystal Palace ***(Football Transfers)***

### MCKENNIE HUYO SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur wamewatangulia Aston Villa katika harakati za kumsajili kiungo wa kati wa Marekani, Weston McKennie mwenye miaka 25 kutoka Juventus . ***(Football Insider)***

### WILLIAMS AITAKA BARCA
WINGA wa Athletic Bilbao, Nico Williams mwenye miaka 21, anaendelea kushikilia uwezekano wa kuhamia Barcelona licha ya kuwa na mazungumzo na Villa, Arsenal, Liverpool na Newcastle United ***(HITC)***

### MATTY CASH AFUATILIWA
MATTY Cash wa Aston Villa tayari anafuatiliwa na AC Milan lakini sasa wapinzani wao Inter Milan wanamfikiria beki huyo wa kulia wa Polannd mwenye umri wa miaka 26, kama anayeweza kuziba nafasi ya mlinzi wa Uholanzi Denzel Dumfries mwenye miaka 28. ***(Sky Sport Italia)***

### WALSH AITAKA ARSENAL
KIUNGO wa kati wa England, Keira Walsh mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kuhamia klabu ya Arsenal . ***(90min)***

### CHELSEA INATAKA MMOJA
CHELSEA inavutiwa na mshambuliaji wa Atletico Madrid, Samu Omorodion na mshambuliaji wa Aston Villa raia wa Colombia Jhon Duran, lakini watamsajili mmoja tu wa wachezaji hao wenye umri sawa wa miaka 20. ***(Fabrizio Romano)***

### DAGUR ANYATIWA NEWCASTLE
NEWCASTLE United ina nia ya kumsajili winga wa Iceland, Jon Dagur Thorsteinsson mwenye umri wa miaka 25 kutoka klabu ya OH Leuven ya Ubelgiji. ***(Chronicle Live)***

### FIKAYO TOMORI KUKATAA
MLINZI wa AC Milan, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 26, huenda akakataa ofa yoyote kutoka kwa Newcastle United msimu huu. ***(Football Insider)***

### HUMMELS KUTUA MALLORCA
BEKI wa zamani wa Ujerumani, Mats Hummels mwenye umri wa miaka 35, anakaribia kusaini mkataba wa kujiunga na Real Mallorca baada ya kuondoka Borussia Dortmund . ***(Diario de Mallorca)***

## DO ZA SOKA MA A ULAYA




# BRUNO GUIMARAES ANUKIA ARSENAL

●●●Beki huyo wa Newcastle amerejea kwenye rada za wababe hao baada ya.....

**LONDON,** ENGLAND

KIUNGO wa Newcastle United, Bruno Guimaraes amerejea katika rada za Arsenal baada ya klabu hiyo kutoridhishwa na majadiliano yao na kiungo wa Hispania, Martin Zubimendi.

Taarifa za awali kutoka vyombo mbalimbali ziliripoti kwamba, Manchester City pamoja na Arsenal hazikuwa tayari kuvunja mkataba wa Mbrazili huyo kumtoa klabuni kwake.

Hata hivyo, Arsenal imeanza kuonesha nia ya kumvuta mchezaji huyo kutua Emirates.

Dili hili huenda likakamilika kwa sababu ya kiuchumi inayopitia Newcastle kwani klabu hiyo wanahitaji kuweka sawa viwango vya mapato na matumizi vya klabu hiyo kulingana na sheria za usawa wa kifedha za Ligi Kuu nchini England.

# UJERUMANI MATUMAINI KIBAO KUBEBA 'EURO 24'

**STUTTGART,** UJERUMANI

KAZI ya Ujerumani ni kuwafanya mashabiki wa nyumbani kuwa na ndoto za Euro 2024, kocha Julian Nagelsmann alisema baada ya ushindi wa 2-0 Jumatano dhidi ya Hungary, akiongeza kwamba anafikiria kushinda mechi inayofuata na si kutazama mbele kwa raundi ya mtoano.

Nagelsmann alisifu kile alichokiita mazingira ya kustaajabisha katika michuano hiyo kwenye ardhi ya nyumbani akitaja matukio wakati wafuasi walipoandamana na timu hadi kwenye basi lao na kuanza kuimba wimbo wa taifa hilo.

"Kulikuwa na sauti kubwa sana uwanjani, hiyo inakupa hisia nzuri," alisema kocha wa Ujerumani na kuongeza, "Hiyo inatusaidia, vigumu kuamini kwa sababu tuna wachezaji wenye uzoefu wa ajabu na wenye mafanikio lakini inafanya jambo la kuvutia."

"Ni jukumu letu kuwaacha mashabiki waendelee kuota."

Mabao ya Jamal Musiala na Ílkay Gündogan yaliipa Ujerumani ushindi murua dhidi ya Hungary ambao ulifanya taifa mwenyeji kuwa timu ya kwanza kufuzu kwa hatua ya mtoano.

Wakiwa na ushindi wa pili mfululizo, Wajerumani hao wana uhakika wa kuwa angalau miongoni mwa timu mbili za juu katika kundi lao baada ya Scotland kutoka sare na Uswisi.

Nagelsmann alikuwa na maneno maalum kwa Musiala, ambaye amefunga katika mechi zote mbili za Ujerumani hadi sasa, akisema anapaswa kupuuza shinikizo na kutoogopa. Mchezaji huyo mwenye miaka 21, anayecheza katika mji wake, aliwapa Wajerumani bao la kuongoza katika dakika ya 22 baada ya safu ya ulinzi ya wapinzani wao kushindwa kuokoa hatari ya mpira uliopigwa na Gündogan, akauwahi na kufunga.

"Anapaswa kucheza tu kama yuko kwenye uwanja mdogo popote pale Ujerumani au Uingereza, haijalishi," alisema Nagelsmann.

"Anapaswa kucheza soka tu na marafiki zake. Asifikirie kuhusu shinikizo, ana kipaji tu cha kucheza soka."

"Tunazidi kuwa bora, lakini tunapoimarika tunapaswa kushinda baadhi ya matatizo," alisema nahodha wa Ujerumani Gündogan.

"Hivyo ndivyo mchezo huu ulivyoonesha leo (juzi) haswa katika kipindi cha kwanza, lakini ndio mashindano, mmenusurika katika hali kama hizi. Tulinusurika na kisha kurudisha nyuma.

"Nilitaka kubaki mvumilivu, kukamilisha kazi zangu bila kujichukulia kwa uzito sana. Kadiri mnavyofanya mazoezi mara kwa mara pamoja, ndivyo hisia za wenzako wa timu pia zinavyokuwa bora, hisia huwa bora nikiwa na vijana wanaonizunguka."

# Juventus, Lazio zamuwania Greenwood

**TURIN,** ITALIA

LAZIO inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Juventus kwa mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood, chanzo kiliiambia ESPN.

Lazio na United wameanza mazungumzo ya kutaka kumnunua Greenwood, ambaye msimu uliopita alicheza kwa mkopo Getafe.

United wanatumaini kukubaliana ada ya takribani pauni milioni 30 ingawa inakubalika kwamba italazimika kupewa ruzuku kwa idadi ya nyongeza kulingana na utendaji.

Lazio walikuwa karibu kusaini Greenwood kwa mkopo mwaka mmoja uliopita kabla ya Getafe kuingilia Kati.

Kwa mujibu wa ripoti, United ingependelea kufanya mazungumzo ya uhamisho wa kudumu msimu huu wa majira ya joto badala ya kukubali uhamisho mwingine wa mkopo. Pamoja na Lazio na Juventus, nia ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 pia imeoneshwa na klabu nyingine za Serie A ikiwemo Napoli.

Pia kumekuwa na nia kutoka kwa klabu za Hispania, Ureno na Ujerumani.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Greenwood na familia yake wako tayari kuhamia nje ya nchi wakati anaendelea kujenga tena kazi yake.

Mhambulizi huyo hajaichezea United tangu Januari 2022 kufuatia kukamatwa kwake kwa tuhuma za kujaribu kubaka na kushambulia. Kesi hiyo ilimalizika Februari 2023.

Mmiliki mwenza mpya wa United, Sir Jim Ratcliffe, alipendekeza Februari mwaka huu kwamba mlango uko wazi kwa Greenwood kuanza tena kazi yake huko Old Trafford, lakini ingawa hakuna kitu ambacho kimekataliwa, chanzo kiliambia ESPN kwamba kuna uwezekano mdogo sana kwa mchezaji huyo kurejea United.

Greenwood alifunga mabao 10 kwa mkopo Getafe msimu uliopita. Getafe, walimaliza katika nafasi ya 12 kwenye LaLiga, wamekuwa na nia ya kumrejesha klabuni hapo lakini hawawezi kufikia mahitaji ya ada ya United.





# Scotland kumkosa Tierney

**COLOGNE,** UJERUMANI

KOCHA wa Scotland, Steve Clarke amesema timu yake bado iko "hai" kwenye Mashindano ya Ulaya baada ya sare ya 1-1 na Uswisi, lakini alikiri Kieran Tierney ataukosa mpambano wao muhimu wa Kundi A dhidi ya Hungary kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Scotland walielekea katika mechi ya Jumatano mjini Cologne dhidi ya Uswisi wakijua walihitaji angalau pointi ili kudumisha matumaini yao ya kutinga hatua ya mtoano ya Euro 2024.

Walipokea kichapo kizito cha 5-1 katika mechi yao ya kwanza dhidi ya Ujerumani.

Scott McTominay aliipa uongozi Scotland dakika ya 13, lakini Xherdan Shaqiri akisawazisha dakika 13 baadaye.

Timu zote zilikuwa na nafasi za kushinda mechi hiyo, huku Grant Hanley akigonga nguzo katika kipindi cha pili na Uswisi ikiwa na juhudi mbili zilizokataliwa kwa kuotea.

Lakini Clarke alifurahishwa na roho ambayo timu yake ilionyesha.

"Ndiyo, ndivyo tulivyotarajia," alisema Clarke. "Hivi ndivyo tumekuwa tukicheza kama timu katika kipindi cha miaka mitatu au minne iliyopita.

"Tulijua kile tulichopaswa kufanya, ulikuwa ni mchezo mzuri wa timu dhidi ya mpinzani mzuri."

"Ilikuwa ni kufanya vyema wakati wote, wakati mwingine haiendi upendavyo," Clarke alisema na kuongeza, "Usiku ule ulikuwa unakaribia kurudi kwenye kile unachofanya vizuri, kufanya kazi kwa bidii."

Lakini Scotland watakuwa bila Tierney kwa mechi yao dhidi ya Hungary Jumapili huko Stuttgart.

Beki huyo wa Arsenal aliumia msuli wa paja kipindi cha pili na kutolewa nje kwa machela.

Alipoulizwa kuhusu Tierney, Clarke alijibu: "Amejeruhiwa, hatacheza mchezo unaofuata kwa hakika."

# RAIS SAMIA KUZINDUA TAMASHA LA KITAIFA LA UTAMADUNI JULAI

**Na Kulwa Mzee**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuzindua tamasha la Kitaifa la Utamaduni lililopangwa kufanyika kwa siku saba kuanzia Julai 20 katika viwanja vya Majimaji mkoani Ruvuma.

Akizungumza na Waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma, alisema tamasha hilo litakuwa la kihistoria, litakusanya tamaduni kutoka mikoa yote Tanzania.

Alisema tamasha hilo linatokana na maagizo ya Rais Samia aliyotoa mwaka 2021 akiwa kwenye ziara mkoani Mwanza.

„Rais aliagiza kufanyika kwa tamasha la Utamaduni kila mwaka ili kurithisha Mali na Utamaduni wa kitanzania.

"Tanzania ina utajiri wa makabila zaidi ya 120, tofauti yake inajenga Umoja na yanaunganishwa na Lugha ya Kiswahili.

"Kudumu kwa Utamaduni inategemea namna unavyorithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine na kwamba urithi wa Utamaduni ni kivutio kikubwa cha utalii, watalii wamevutiwa sana,"alisema Mwinjuma.

Aidha, alisema tamasha hilo litakuwa tofauti na matamasha mengine mawili yaliyowahi kufanyika mwaka 2022 na 2023 kwani litakuwa na sura ya Kitaifa na litakuwa chini ya Wizara husika.

Waziri Mwinjuma alisema jukumu la rasilimali fedha litakuwa chini ya Sekta Binafsi ambayo ni Kampuni ya Drum-Beat Carnival (Tz) Limited itakayosaidia pia kuhamasisha tamasha liwe na hadhi kubwa.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Jangwani jijini Dar es Salaam, wakicheza mpira katika Uwanja wa Jakaya Kikwete hivi karibuni kama walivyokutwa na mpiga picha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam Complex kuwekwa viti kwa ajili ya Ligi ya Mabingwa

**Na Adam Fungamwango**

UWANJA wa Azam Complex, uliopo Chamazi, Dar es Salaam, unatarajiwa kuwekwa viti wiki hii kwa ajili ya kuuwezesha kutumika kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Thabit Zacharia, amesema pamoja na mambo mengine, ukarabati huo unalenga zaidi kuuwezesha uwanja ukidhi mahitaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Africa (CAF) ili kuruhusiwa kuchezewa michuano hiyo ya kimataifa.

Azam msimu huu itashiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, baada ya kushika nafasi ya pili kwenye msimamo Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika hivi karibuni.

"Tayari tumeshaleta viti, ndani ya wiki hii vitaanza kufungwa uwanja mzima. Kwa maana hiyo uwanja upo kwenye maboresho na Ligi ya Mabingwa msimu ujao itapigwa hapo," alisema Thabit, maarufu mama Zaka Zakazi.

Alisema hayo yote ni kuhakikisha klabu inakuwa na miundombinu ya uhakika na viti bora kama ambavyo wamekuwa hivyo miaka yote.

Awali uwanja huo ulikuwa unatumika kwenye michuano ya kimataifa, lakini baadaye CAF ilikuja na muongozo mpya, ikitaka viwanja vyote vitakavyochezewa michezo ya kimataifa kuwa na viti vya kukalia mashabiki, kitu ambacho kilikosekana katika uwanja huo ambao sehemu za kukaa mashabiki zimetengenezwa kwa mtindo wa mabenchi.

Hali hiyo ilipeleka CAF kuufungia uwanja huo, na athari zilionekana kwa klabu za Simba na Yanga msimu uliopita zilipokuwa zinahangaika kupata sehemu ya kucheza mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya Uwanja wa Benjamin Mkapa kufungwa kutokana na matengenezo.

Busara ya serikali ndiyo iliyotatua tatizo hilo na kwa kuziruhusu kucheza michezo ya kimataifa tu kwenye uwanja wa Mkapa.

## Bodi ya Ligi Kuu kuja na dawa wamiliki

INATOKA UK. 24

Singida.

Mbali na hilo, baadhi ya wachezaji wa Singida Fountain Gate nao walipelekwa kwenye klabu ya Ihefu ambayo kwa sasa imebadilishwa jina ikiitwa Singida Black Stars ambapo pia Ofisa Mtendaji huyo alisema kuwepo kwa kanuni itakayofanya kazi, ndiyo ,muarobaini' wa kuzuia mambo hayo.

Kuhusu mmiliki mmoja kuwa na timu mbili alisema lipo na limekuwa kilipigiwa kelele, lakini kwa bahati mbaya hawapati uthibitisho wowote wa kimaandishi kwenye hati ya umiliki.

"Hili la ndani ya ligi kuna mtu anamiliki zaidi ya klabu moja, tabu tunayoipata ukienda kwenye hati ya umiliki huioni, na huwezi kumpata na sisi tunafanya kazi kwa nyaraka siyo hisia, kisheria wanakushinda, lakini hili limezua mjadala mkubwa, sasa kuthibitisha ndiyo changamoto, lakini siyo kwamba wenzetu wa Idara ya Sheria wameliacha iendelee, hapana, bado wanatafuta namna ya kupambana nalo, ikiwemo kufuatiliwa mienendo yao ya kifedha ya klabu husika na wataalam wa kazi hizo, pamoja na chochote ambacho wataona kinaweza kuwawezesha kutambua mtu mmoja anajihusisha na klabu mbili kwenye ligi moja," alisema Kasongo.

Mbali na malalamiko hayo, pia kumeibuka maswali mengi juu ya udhamini wa klabu kwa kampuni au mtu mmoja kudhamini klabu zaidi ya moja ndani ya Ligi ambalo pia litafanyiwa kazi.

Kasongo, alisema wanaenda kufanyia kazi kila dosari walizoziona au au maeneo yanayopigiwa kelele na wadau ili kuwa na Ligi bora zaidi na imara.

Eneo lingine ambalo limekuwa likipigiwa kele na bodi hiyo ya Ligi imesema itaanza kutunga kanuni kudhibiti ni eneo la vitendo vya kishirikina na adhabu zake

## Simba yaanika sababu kuwaacha Miquissone, Kenedy

INATOKA UK. 24

dakika ya 89 kwenye mchezo dhidi ya Namungo liliwakera viongozi na benchi la ufundi la klabu hiyo.

"Kenedy licha ya kupata nafasi ya mara kwa mara ya kucheza msimu uliomalika, kiwango chake hakikukuwa, amekuwa mchezaji wa kawaida na mwenye makosa mengi ndani ya uwanja, labda kama atapata timu nyingine atakuza kiwango chake," alisema Msemaji huyo.

Juzi jioni, Simba ilitoa taarifa ya kumuacha Kenedy na Miqussone na kuungana na Shaban Chilunda, John Bocco, Saido Ntibanzokiza kufikisha idadi ya wachezaji watano waliotangazwa kuachwa na timu hiyo.

Klabu hiyo kupitia kwa Menaja habari wake, Ahmed Ally alisema wataendelea kuwatangaza wachezaji wanaochana nao kabla ya kuanza kuwatangaza wale wanaowasajili kwa ajili ya msimu ujao

Michezo
Nipashe

## Bruno Guimaraes anukia Arsenal



UKURASA 21



Beki wa kati wa timu ya taifa ya Ujerumani, Antonio Rudigar (kushoto) akiwania mpira na mshambuliaji wa Hungary, Roland Sallai katika mchezo wa Kundi A kwenye fainali za ‚Euro 2024‘ juzi usiku nchini Ujerumani, wenyeji walishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# BODI YA LIGI KUU KUJA NA DAWA WAMILIKI TIMU ZAIDI YA MBILI

●●●Pia kupiga ‚stop‘ tabia za klabu kuhama makazi na umiliki ndani ya msimu mmoja...

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Ligi Kuu imesema imeandaa mchakato wa kanuni kuzuia mtindo wa baadhi ya klabu kuhama mkoa mmoja kwenda mwingine katikati ya msimu pamoja na mtu au taasisi kumiliki timu zaidi ya moja kwenye Ligi Kuu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Almasi Kasongo, amesema kazi hiyo inafanywa na Kamati ya Sheria ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), ambayo itatengeneza kanuni ya kuzuia tabia hiyo ya klabu kuondoka kwenye mkoa mmoja kwenda mwingine ndani ya msimu na kubadilisha jina.

"Timu ilikuwa ya Mbeya, lakini ghafla imekuwa ya Shinyanga, mara inatoka Shinyanga inakwenda Tanga ndani ya msimu mmoja, hii si sawa, wenzetu wa Idara ya Sheria wanalifanyia kazi. Nafikiri sasa hivi tupo katika maboresho ya kanuni, watakuja na kitu ambacho kitamaliza kabisa au kupunguza mambo haya, „ alisema Kasongo.

Msimu uliomalizika hivi karibuni klabu ya Singida Fountain Gate, ilihama kutoka Singida na kuhamia Mwanza, huku Ihefu ikihama kutoka Mbarali, Mbeya kwenda

INAENDELEA UK. 23

## Simba yaanika sababu kuwaacha Luis Miquissone, Kenedy Juma

**Faustine Feliciane na Adam**

**Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Simba kushuka kiwango na gharama kubwa ya mshahara ni sababu mojawapo ya kuamua kuachana na baadhi ya wachezaji wao kwenye kikosi hicho.

Inalezwa winga Luis Miquissone ni mchezaji aliyekuwa aklilipwa fedha nyingi kutokana na mkataba wake aliosaini wakati akirejea mara ya pili kwenye klabu hiyo akitokea Al Ahly ya Misri.

Mmoja wa viongozi ndani ya klabu hiyo aliiambia Nipashe kuwa, licha ya mshahara mkubwa aliokuwa akipokea, Miquissone hakuwa na mchango wowote ndani ya klabu hiyo akimaliza msimu bila kwenye Ligi Kuu.

"Simba ilikuwa inamlipa fedha nyingi za mshahara, lakini nadhani wanasimba wenye mashahidi, hata pale alipopewa nafasi hakuonyesha makali yake ambayo wanasimba wengi walikuwa na mategemeo naye," alisema kiongozi huyo na kuongeze, "Nikukumbushe tu Luis alirejea Simba Julai 22, mwaka jana akitokea Al Ahly, amecheza hapa kwa msimu mmoja tu, hakuwa na makali kama aliyoyaonyesha awali alipojiunga nasi, hajafunga bao lolote hadi msimu unamalizika, halafu ni miongoni mwa wachezaji wanaolipwa pesa nyingi ndani ya kikosi, hii tumeona si sawa, tumeamua tuachana naye," alisema kiongozi huyo.

Mchezaji huyo, awali alijiunga na Simba 2020 na kucheza kwa msimu mmoja ambao ulikuwa na mafanikio makubwa, akiiwezesha timu hiyo kutwaa ubingwa, kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa akifunga baadhi ya mabao yaliyoiwezesha kufika hapo, ikiwemo kupachika bao pekee dhidi ya Al Ahly ya Misri, Februari 23, 2021.

Kiwango hicho kilimuwezesha kusajiliwa na Al Ahly, ambako hakuwa na wakati mzuri na kujikuta akirejea tena nchini msimu uliopita.

Alisema kwa upande wa Kenedy ni kiwango duni alichokionyesha huku akiwa na makosa mengi kwenye uchezaji ndio sababu ya kuachana naye na kumpa fursa ya kwenda sehemu nyingine kucheza.

Alisema bao la kujifunga la

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042